# Maswali Matatu ya Mkristo Mmoja
# Na
# Majibu Yake

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LTD

# Maswali Matatu ya Mkristo Mmoja na Majibu Yake

**Tafsiri ya Kiswahili ya:**
Ek Isaa'i ke Tiin Sawaal aur un ke Jawaabaat (Kiurdu)

Ek Īsā'ī ke Tīn Sawāl aur un ke Jawābāt (Swahili Translation)

**Mwandishi:**
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

**Mfasiri:**
Sheikh Mussa Issa Mashiri

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1892
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2025

© Islam International Publications Ltd.

**Kwa Maelezo Zaidi:**

**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

**ISBN:** 978-1-84880-717-4
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

## Neno la Mwenezi

Mnamo Mei-Juni 1889, Mkristo mmoja, Abdullah James, aliipelekea Anjuman Himayate Islam, Lahore, (Chama cha Waislamu-Suni) maswali matatu kuhusiana na Islam ili kujibiwa. Anjuman kwa kuelewa sana kwamba huu ndio uwanja wa Waahmadiyya pekee, ikayatuma maswali hayo kwa Mwanzilishi wa Jumuiya Ahmadiyya Seyidna Ahmad[as] na masahaba zake wawili, Maulana Hakiim Nuru-Din[ra] na Maulawii Ghulam Nabii[ra].

Seyidna Ahmad[as] na masahaba zake hao wakaandika majawabu ya kuridhisha sana, ambayo Anjuman hiyo ikayachapisha.

Baadaye, Jumuiya Ahmadiyya ikatoa majibu yaliyo-andikwa na Seyidna Ahmad[as] kwa sura ya kitabu. Na kitabu hicho kimefasiriwa sasa kwa Kiswahili na Sheikh Mussa Issa. Sheikh Khurram Shahzad akaidurusu. Na kabla ya kuipeleka mtamboni nikaisoma kwa uangalifu ili kuisogeza karibu zaidi na lugha chanzo.

Maswali yenyewe na majibu yao mkiyasoma kwa makini mtaongezeka elimu ya dini na imani; nayo yatosha sana kumwongoza Mkristo.

Sheikh Ansar Hussain alizipanga herufi zake kwa kompyuta na kutengeneza fomati. Wote wahusika na

kazi hii tukufu wanashukuriwa. Mwenyezi Mungu Awaongoze wenye bahati njema kwa kupitia kitabu hiki.

Hili ni tunda jipya tena la *Dawati la Kiswahili*.

Jamil R. Rafiq
Wakilut-Tasnif
Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan 30 Mei 2024

Jalada la chapa ya kwanza

يا أيها الذين آمنوا قوا أنفسكم وأهليكم نارا

اے ایمان والو اپنے آپ کو اور اپنے اہل و عیال کو دوزخ کی آگ سے بچاؤ

# ایک عیسائی کے تین سوال

# اور اُن کے جوابات

جسے

## انجمن حمایت اسلام لاہور نے

## سنہ ۱۳۰۹ ہجری المقدس

علی صاحبہا التحیہ والسلام

مطبع گلزار محمدی لاہور میں منشی گلزار محمد مالک مطبع کے اہتمام سے چھپوایا

رجسٹری شدہ ہے۔ بے اجازت کوئی نہ چھاپے

Tafasiri ya jalada la chapa ya kwanza




# Maswali Matatu ya Mkristo Mmoja

# Na Majibu Yake

## Ambayo

## Anjuman Himayate Islam, Lahore

## imechapisha mnamo mwaka 1309 Hijra tukufu

*Maamkizi na salamu juu ya Mhamaji*

**katika Matbaa Gulzar Muhammadi Lahore chini ya usimamizi wa Munshi Gulzar Muhammad mmliki wa kiwanda cha uchapishaji**.

Kimesajiliwa. Asikichapishe yeyote bila ruhusa.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ [1]

نَحْمَدُهٗ وَنُصَلِّيْ عَلٰى رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ [2]

بَلْ هُوَ اٰيٰتٌۢ بَيِّنٰتٌ فِيْ صُدُوْرِ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْعِلْمَ [3]

Siku chache zilizopita, Mkristo mmoja aitwaye Abdullah James, alituma maswali machache kwa Anjuman, yanayohusiana na Islam ili kupata majibu. Majibu ya haya maswali yameandikwa na wasaidizi watatu Mabingwa waheshimiwa wa Anjuman, ambayo yanachapishwa kwa shukrani yote katika kitabu hiki.

## Maswali

**La Kwanza:** Muhammad[saw] kushuku unabii wake na Kurani Tukufu kuwa Neno la Mungu, kama ilivyoandikwa katika Sura Al-Baqara na Sura Al-An‘aam: فَلَا تَكُوْنَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِيْنَ[4] . Hii inathibitisha kwamba Mtume[saw] alikuwa na yakini kwamba yeye si mtume wa Mungu. Kama kweli angalikuwa mtume wa Mungu, au

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

[2] Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume wake karimu.

[3] Bali hizi ni Aya waziwazi (zinazohifadhiwa) katika vifua vya wale waliopewa elimu. Al-‘Ankabuut 29:50

[4] Basi usiwe miongoni mwa wafanyao shaka. Al-Baqara 2:148, Al-An‘aam 6:115

angekuwa ameonyesha muujiza wowote, au tukio la miraji lingalikuwa limetokea kweli, au Kurani Tukufu ingalikuwa imeletwa na Jibril[as], basi kamwe asingelikuwa na shaka juu ya utume wake. Kwa hiyo inathibitika shaka yake waziwazi juu ya Kurani Tukufu na utume wake, basi yeye hakuwa mtume wa Mungu.

**La Pili:** Muhammad[saw] hakupewa muujiza wowote kamwe, kama ilivyoelezwa katika Sura Al-'Ankabuut. (Tafsiri ya Kiarabu): Na wanasema; kwa nini hakuteremshiwa baadhi ya ishara kutoka kwa Mola wake? (Yaani, hata ishara moja, kwani neno *la* lililomo katika Aya lakanusha kitu kinachoitwa ishara). Na ipo katika Sura Banii Israaiil pia: Na Tumeacha kuzituma ishara kwa sababu watu wa zamani walizikadhibisha. Hii yaonyesha wazi kwamba Mungu Hakumpa muujiza wowote. Kwa hakika kama angepewa japo muujiza mmoja tu, kamwe asingekuwa na shaka juu ya utume wala juu ya Kurani Tukufu.

**La Tatu:** Kama kweli Muhammad[saw] angalikuwa mtume, asingesema akishindwa kujibu maswali ya wakati ule kwamba, Mungu ndiye Anajua; yaani mimi sijui; wala asingeongopa kuhusiana na watu wa Pango juu ya idadi yao, wala asingesema kwamba jua linachwea au linazama katika chemchem iliyovurugika, kwani jua

ni kubwa mara milioni 90 kuliko ardhi, sasa inawezaje lizame kwenye chemchem iliyovurugika?[5]

[5] Tanbihi: Hadhrat Masihi Mau'udi[as] amejibu swali la tatu la Abdallah James kwa kulifanya la pili (labda kutokana na umuhimu wake), na ameliweka swali li pili mwishoni, wakati Hadhrat Khalifa tul Masih I amezingatia mpangilio wa maswali ya Abdallah James. Mwenezi

# Majibu Kutoka kwa Ateremkiwaye Baraka za Rahmani, Chanzo cha Nuru za Kurani, Janabi Mirza Ghulam Ahmad[as], Chifu wa Qadian

## Jibu kwa Swali la Kwanza

Mpinzani, kwa ajili ya kutilia nguvu dai lake, kwanza ametoa aya moja kutoka Sura Al-Baqara ambayo maneno yake kamili ni haya: اَلْحَقُّ مِنْ رَّبِّكَ فَلَا تَكُوْنَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِيْنَ[6]. Kwa kuangalia muktadha wa aya hii, yaani kwa kutazama aya za mbele yake na nyuma yake inadhihirika wazi kwamba hakujatajwa hapo utume wala Kurani Tukufu, bali imeelezwa kuwa kuanzia sasa si kuelekea Baitul-Mukaddas, bali kwa kuelekea Kaaba mnatakiwa kusali. Hivyo basi, katika aya hii Allah Mtukufu Anasema kuwa hii ndiyo haki, yaani kusali kwa kuelekea Kaaba ndiyo haki, jambo lililowekwa toka mwanzo, nalo limeelezwa pia kwenye Vitabu vya zamani kama utabiri. Basi (Ewe msomaji wa Kitabu hiki) usiwe miongoni mwa wenye shaka.[7] Tena aya zinazofuatia zinaendelea kueleza habari

---

[6] Haki ndiyo iliyotoka kwa Mola wako, basi usiwe miongoni mwa wafanyao shaka. Al-Baqara 2:148

[7] Hii inaashiria kwamba kwenye Vitabu vya zamani na pia katika Injili, vipo vidokezo vya habari za kugeuzwa kwa Kibla. Angalieni Yohana 4:21-24. Imeandikwa kwamba: Yesu akamwambia, mama, unisadiki, saa inakuja ambayo hamtamuabudu Baba katika mlima huu, wala kule Yerusalemu.

hii hii. Allah Mtukufu Anasema: وَ مِنۡ حَيۡثُ خَرَجۡتَ فَوَلِّ وَجۡهَكَ شَطۡرَ الۡمَسۡجِدِ الۡحَرَامِ ؕ وَ اِنَّهٗ لَلۡحَقُّ مِنۡ رَّبِّكَ[8] — yaani, popote utokapo geuza uso wako kuelekea Kaaba, bila shaka hiyo ndiyo haki itokayo kwa Mola wako. Ilmuradi, iko wazi kabisa kwamba aya hizi zote zinahusu habari ya Kaaba tu, hazihusu jambo jingine lolote. Na kwa kuwa agizo hili la kuelekea Kaaba katika sala ni amri kwa ujumla kuhusiana na Waislamu wote, hivyo, kutokana na amri ya kawaida, kwa ajili ya kuondoa shaka ya baadhi ya watu wenye tabia ya wasiwasi, wametulizwa katika aya hizi ya kuwa jambo hili lisiwahangaishe kwamba kwanza — kuendelea kusali kuielekea Baitul-Mukaddas kwa sababu gani wameanza kusali kwa kuelekea kwenye Kaaba? Basi, Amesema kwamba hili si jambo jipya, bali ni jambo lile lile lilokadiriwa, Aliloishahabarisha Mwenyezi Mungu toka mwanzo kupitia Mitume wake wa zamani. Kwa hiyo msiwe na shaka kuhusu hilo.

Aya ya pili aliyoandika mpinzani mwenyewe kwa ajili ya kuthibitisha madai yake ni aya moja ya Sura Al-An‘aam ambayo pamoja na Aya zingine husika ipo hivi kama ifuatavyo: اَفَغَيۡرَ اللّٰهِ اَبۡتَغِىۡ حَكَمًا وَّ هُوَ الَّذِىۡۤ اَنۡزَلَ اِلَيۡكُمُ الۡكِتٰبَ مُفَصَّلًا ؕ وَالَّذِيۡنَ اٰتَيۡنٰهُمُ الۡكِتٰبَ يَعۡلَمُوۡنَ اَنَّهٗ مُنَزَّلٌ مِّنۡ رَّبِّكَ بِالۡحَقِّ فَلَا تَكُوۡنَنَّ مِنَ الۡمُمۡتَرِيۡنَ[9]. Yaani, je nimtafute Mwamuzi ghairi ya Allah, naye Ndiye Amewateremshieni Kitabu kielezacho waziwazi? Na wale tuliowapa

---

[8] Al-Baqara 2:150

[9] Al-An‘aam 6:115

Kitabu, yaani Kurani — mradi wake ni wale tuliowafahamisha elimu ya Kurani — wanajua vyema kwamba hicho kimetoka kwa Allah, basi ewe msomaji usiwe miongoni mwa wenye shaka.

Sasa, kwa kuziangalia aya hizi inaonekana wazi kwamba waliotajwa katika aya hii, فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِينَ[10] , ni wale tu walio na sehemu ndogo katika yakini, imani na elimu; bali inadhihirika, kutokana na aya za juu hii, pia kwamba hapa agizo hili la 'usiwe miongoni mwa wanye shaka' ni kauli ya Mtume[saw] ambayo imetajwa na Kurani Tukufu. Kwani katika aya ya mwanzo ambayo aya hii inahusiana nayo, ni kauli ya Mtume[saw] tu, yaani hii kwamba أَفَغَيْرَ اللّٰهِ أَبْتَغِي حَكَمًا[11] . Basi tafsiri kwa lugha safi ya aya zote hizi ni hii kwamba ghairi ya Mwenyezi Mungu siwezi kumfanya yeyote kuwa Mwamuzi baina yangu na nyinyi, kwani Yeye Ndiye Aliyewateremshieni Kitabu kielezacho waziwazi. Basi, waliopewa elimu ya Kitabu wanajua vizuri kwamba hiki Kitabu kimetoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo (Ewe mtu usiyejua) usiwe miongoni mwa wenye shaka.

Sasa, ni dhahiri kutokana na uchunguzi kwamba Mtume[saw] mwenyewe hana shaka, bali anawakataza wale waliokuwa na shaka kwa ushahidi na dalili. Hivyo licha

[10] Usiwe miongoni mwa wenye shaka.

[11] Je nimtafute Mwamuzi ghairi ya Allah.

ya kauli bayana hiyo kumnasibishia Mtume[saw] shaka juu ya Utume wake, kama si kutojua na ukosefu wa elimu au chuki tupu ni nini basi!

Kama fikara izuke moyoni mwa mtu kwamba kama Waislamu wapya au wenye wasiwasi walikuwa wanakatazwa waliokuwa na imani dhaifu, hapo ingefaa kusemwa kuwa "ninyi msiwe na shaka" badala ya "wewe usiwe na shaka", kwani mwenye imani dhaifu hawi mtu mmoja tu bali wanakuwa wengi; badala ya wingi kwa nini neno la umoja limetumika, basi jibu lake ni hili kwamba umoja huu ndio umoja wa jinsi (kundi) ambao humaanisha 'wingi'. Kama mkisoma Kurani Tukufu kuanzia mwanzo mpaka mwisho mtakuta ndani yake matumizi kama haya kwamba sehemu nyingi inaita kundi la watu kama mtu mmoja, mathalan, tazameni aya hizi kama mfano: لَا تَجْعَلْ مَعَ اللّٰهِ اِلٰهًا اٰخَرَ فَتَقْعُدَ مَذْمُوْمًا مَّخْذُوْلًا ۔ وَ قَضٰى رَبُّكَ اَلَّا تَعْبُدُوْٓا اِلَّآ اِيَّاهُ وَ بِالْوَالِدَيْنِ اِحْسَانًا ؕ اِمَّا يَبْلُغَنَّ عِنْدَكَ الْكِبَرَ اَحَدُهُمَآ اَوْ كِلٰهُمَا فَلَا تَقُلْ لَّهُمَآ اُفٍّ وَّ لَا تَنْهَرْهُمَا وَ قُلْ لَّهُمَا قَوْلًا كَرِيْمًا ۔ وَ اخْفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ الذُّلِّ مِنَ الرَّحْمَةِ وَ قُلْ رَّبِّ ارْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيٰنِيْ صَغِيْرًا ۔[12]

Yaani usifanye Mungu mwingine pamoja na Allah usije ukalaumiwa na kutupwa. Na Mola wako Anataka usimwabudu yeyote ila Yeye tu, asiwe muabudiwa wako minghairi yake Yeye, na ufanye wema kwa wazazi. Kama mmoja wao akifikia uzee pamoja nawe, au wote

---

[12] Banii Israaiil 17:23-25

wawili, basi usiwambie hata 'akh', wala usiwakemee, na useme nao kwa msemo wa kuonyesha heshima na taadhima. Na uwainamishie bawa lako kwa unyeyekevu na huruma. Na useme: Mola wangu, uwarehemu kama walivyonilea katika utoto wangu.

Sasa, angalia katika aya hizi mwongozo uko wazi kabisa kwamba neno la umoja linahusikana na kundi la umati, walioitwa kwa neno 'wewe' baadhi ya wakati katika aya hizi. Siye Mtume[saw] anayeambiwa katika aya hizi, kwa sababu ndani ya aya hizi mna agizo kuhusu kuwaheshimu, kuwatii na kuwatendea wazazi kwa wema na hisani, na ni wazi kwamba wazazi wa Mtume[saw] walikwishafariki utotoni bali katika umri wa kunyonya. Hivyo, hapa na penginepo inathibitika kinagaubaga kwamba ni msemo wa kawaida wa Kurani Tukufu kueleza neno la umoja kuhusu kundi, na njia hii inaendelea toka mwanzo hadi mwisho. Njia hii hii ya kusema imetumika ndani ya maagizo ya Torati pia, kwamba agizo linatolewa kwa neno la umoja, lakini humaanisha wana wote wa Israeli. Kwa mfano, katika Kutoka mlango wa 33 na 34, Musa kidhahiri anaambiwa: (mstari 11), Zingatia kila hukumu ninayokuagiza siku ya leo. (12): Ujihadhari nafsi yako, usije ukafanya agano na wenyeji wa nchi ile unayoiendea. (17): Usifanye miungu ya kuyeyusha.

Sasa, kwa kuangalia sehemu za mbele na nyuma ya aya hizo, inabainika kwamba Nabii Musa[as] ndiye anayeamrishwa, lakini ukweli ni kwamba amri hizi hazimuhusu Hadhrat Musa[as]. Hadhrat Musa[as] hakuwahi kwenda Kanaani, wala tendo analokatazwa kama kuabudu masanamu haliwezi kutendwa na mja wa Mungu, mcha Mungu, kama Nabii Musa, mvunja masanamu. Kwani, Musa[as] ni yule mpendwa wa Mwenyezi Mungu ambaye kuhusu shani yake katika mlango huu huu Mwenyezi Mungu Amesema: Nitafanya na neno hili ulilolinena. Nami nakujua jina lako. (Kutoka 33:17)

Basi, ikumbukwe kwamba hii ndiyo njia ya Kurani. Katika sehemu nyingi za Kurani Tukufu na Torat amri zinatolewa kwa njia hii, kana kwamba wanaambiwa Hadhrat Musa[as] na Mtume[saw], lakini kwa hakika wanaambiwa watu wa kaumu na umati. Lakini asiyeelewa njia ya Vitabu hivyo, anafikiri kwa sababu ya kukosa ujuzi kwamba nabii anayeteremshiwa maneno hayo ndiye anaambiwa na kukaripiwa. Lakini kwa kutafakari na kuuchunguza muktadha inabainika kwamba wazo hili ni kosa tupu.

Tena, upinzani huu unang'olewa mbali kwa kuzichunguza aya hizi Alimosifu Mwenyezi Mungu yakini kamili ya Mtume[saw], kama Asemavyo Mwenyezi

Mungu sehemu moja: قُلْ اِنِّيْ عَلٰى بَيِّنَةٍ مِّنْ رَّبِّيْ[13] (Juzuu 7). Yaani sema: Hakika mimi ninayo dalili wazi itokayo kwa Mola wangu. Kisha, sehemu nyingine Anasema قُلْ هٰذِهٖ سَبِيْلِيْٓ اَدْعُوْٓا اِلَى اللّٰهِ عَلٰى بَصِيْرَةٍ[14] (Juzuu 13). Yaani, sema, hii ndiyo njia yangu, ninaita kwa Allah kwa ujuzi hasa. Tena sehemu nyingine Anasema وَ اَنْزَلَ اللّٰهُ عَلَيْكَ الْكِتٰبَ وَ الْحِكْمَةَ وَ عَلَّمَكَ مَا لَمْ تَكُنْ تَعْلَمُ ؕ وَ كَانَ فَضْلُ اللّٰهِ عَلَيْكَ عَظِيْمًا[15] (Juzuu 5). Yaani, Allah Amekuteremshia Kitabu na hekima, yaani Amekudhihirishia dalili za ukweli wa Kitabu na ukweli wa Utume wako, na Amekufundisha maarifa yale uliyokuwa huwezi kuyajua wewe mwenyewe, na fadhili ya Allah iliyo juu yako ni adhimu. Kisha katika Sura An-Najm Anasema: مَا كَذَبَ الْفُؤَادُ مَا رَاٰى[16] مَا زَاغَ الْبَصَرُ وَ مَا طَغٰى ۔ لَقَدْ رَاٰى مِنْ اٰيٰتِ رَبِّهِ الْكُبْرٰى[17] . Yaani, moyo wa Mtume[saw] haukuzikadhibisha ishara za kimbingu zibainishazo ukweli wake baada ya kuziona, yaani hakuzitilia shaka. Jicho halikupotoka kulia wala kushoto, wala halikuvuka mipaka, bali lilitulia kwenye haki, na akaziona ishara za Mungu wake zilizokuwa kubwa kabisa.

---

[13] Al-An'aam 6:58

[14] Yuusuf 12:109

[15] An-Nisaa 4:114

[16] An-Najm 53:12

[17] An-Najm 53:18-19

Enyi wasomaji, angalieni kwa adili. Enyi wapenda haki, tafakarini kidogo kwa uadilifu, jinsi Mwenyezi Mtukufu Anavyoeleza kinagaubaga kwamba Mtume[saw] alikuwa na yakini kamili juu ya utume wake kwa busara kamili, na akaonyeshwa ishara kubwa sana.

Basi muhutasari wa jawabu ni kwamba hamtakuta ndani ya Kurani Tukufu nzima chochote wala lolote kudokeza kuwa Mtume[saw] alikuwa na shaka juu ya Utume wake au Kurani Tukufu kuhusu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Bali, hakika halisi kabisa ni kwamba, kwa kadiri ya yakini kamili, busara kamili, maarifa kamili na ujuzi kamili sana aliyodai Mtume[saw]kuhusu dhati yake yenye baraka na kisha akaithibitisha, haupatikani uthibitisho kamili kama huo ndani ya Kitabu chochote kingine kilichopo. فَهَلْ مَنْ يَسْمَعُ فَيُؤْمِنُ بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهِ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَيَكُوْنُ مِنَ الْمُسْلِمِيْنَ الْمُخْلِصِيْنَ[18]

Ibainike kwamba ndani ya Injili[19] zimeelezwa baadhi ya kauli za Hadhrat Masihi[as] ambazo kwa kuzingatia kwa makini inajulikana wazi kwamba Hadhrat Masih[as] katika siku za mwisho wa umri wake aliingiwa na shaka kidogo kuhusu unabii wake na kusaidiwa na Mwenyezi Mungu, kama maneno haya, kana kwamba yalikuwa ni maneno

---

[18] Basi, je yupo anayesikia halafu anamwamini Allah na Mtume wake Muhammad[saw] na anakuwa miongoni mwa Waislamu wenye ikhlasi?

[19] Hizi shaka zinaibuka katika Injili zote nne, hususani Injili ya Mathayo ndiyo iliyotia shaka ya hali ya juu sana.

ya mwisho, Eloi, Eloi, lama sabaktani, ambayo maana yake ni Ee Mungu wangu, Ee Mungu wangu mbona umeniacha? Katika wakati hasa wa kuaga dunia — ambao huwa wa kudhihiri kwa nuru za yakini na imani ya waja wa Mungu, yakatoka maneno haya kinywani mwake. Vilevile ilikuwa ni desturi yake kupakimbia pale alipohisi nia mbaya ya maadui zake, ilhali tayari alikuwa ameshapata ahadi ya kulindwa na Mwenyezi Mungu. Kwa mambo haya mawili shaka na wasiwasi upo dhahiri. Kisha, kulia usiku kucha kuhusu jambo alilojua mapema mwisho wake mbaya, kunamaanisha nini isipokuwa kwamba alikuwa na shaka tupu katika kila jambo.

Mambo haya yote yameandikwa kwa kuiondolea mbali shutuma hii ya Wakristo, waila tunaweza kumwondolea mbali mpendwa wetu Masihi[as] – ambaye hakuepukana na unyonge na udhaifu wa kibinadamu – lawama hizi zote mara moja kwa ukanusho mmoja tu wa Uungu na Uana, lakini ndugu zetu Wakristo watakabili shida sana.

## Jibu la Swali la Pili

Ibainike wazi kwamba lengo la mpinzani kwa kuleta aya hizo mbili ili kukanusha miujiza, halithibitiki katu, bali kinyume chake inathibitika kwamba lazima iliendelea kudhihiri miujiza ile kwa Mtume[saw] inayotakiwa kudhihiri kwa Mtume mkweli na mkamilifu. Hii itabainika vizuri na maelezo ya hapa chini.

Aya ya kwanza aliyoifasiri mpinzani kwa kutilia nguvu madai yake kuitenganisha na ibara zile husika, pamwe na aya zingine zinazofafanua muradi wenyewe, ni hii:

وَ قَالُوْا لَوْ لَآ اُنْزِلَ عَلَيْهِ اٰيٰتٌ مِّنْ رَّبِّهٖ ؕ قُلْ اِنَّمَا الْاٰيٰتُ عِنْدَ اللّٰهِ ؕ وَ اِنَّمَآ اَنَا نَذِيْرٌ مُّبِيْنٌ ۔ اَوَ لَمْ يَكْفِهِمْ اَنَّآ اَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتٰبَ يُتْلٰى عَلَيْهِمْ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَرَحْمَةً وَّ ذِكْرٰى لِقَوْمٍ يُّؤْمِنُوْنَ ۔[20] ... وَ يَسْتَعْجِلُوْنَكَ بِالْعَذَابِ ؕ وَ لَوْ لَآ اَجَلٌ مُّسَمًّى لَّجَآءَهُمُ الْعَذَابُ ؕ وَ لَيَاْتِيَنَّهُمْ بَغْتَةً وَّ هُمْ لَا يَشْعُرُوْنَ[21]

Yaani, wanasema, kwa nini hakuteremshiwa ishara, yaani zile ishara (mnazoziomba, yaani ishara za adhabu), hizo ziko kwa Mwenyezi Mungu na ziko katika uwezo wake wa kutekeleza. Na mimi ni mwonyaji tu, yaani kazi yangu ni kuwa nionye na siku ya adhabu, siyo niteremshe adhabu mwenyewe. Tena Amesema, je kwa watu wale (wanaotaka kuteremshiwa ishara ya adhabu) haiwatoshi ishara ya rehema kwamba tumekuteremshia (Ee Mtume uliye Ummi) Kitabu (chenye sifa zote kamilifu) kile wanachosomewa, yaani Kurani Tukufu iliyo ishara ya rehema ambayo kwa hakika yamaanisha shabaha ile wanayotaka kutimiza kwayo makafiri wa Makka kwa ishara ya adhabu. Kwani makafiri wa Makka walioomba ishara ya adhabu ili kwa kuwaangukia iwafikishe kwenye yakini hasa, kisiwe ni kitu cha kuonekana tu, kwani katika ishara za kushuhudia kwa macho tu kulikuwa na uwezekano wa ulaghai au wazo la

20 Al-'Ankabuut 29:51-52

21 Al-'Ankabuut 29:54

'kuloga macho'. Basi kwa kuondoa shaka na wasiwasi huu, Akasema, mkitaka ishara itakayowaangukieni, basi kuna haja gani ya ishara ya adhabu? Je haitoshi ishara yenye rehema kwa kupata shabaha hii — yaani Kurani Tukufu itiayo kiwi machoni mwenu kwa mionzi mikali, na iliyojaa nuru, na inadhihirisha mazuri yake, kweli zake, maarifa na sifa zake mahususi zisizo za kawaida, ambayo mmeshindwa kuikabili na kushindana nayo. Nayo inawaathirini kiajabu ninyi na watu wenu[22], na

[22] Hizi sifa za ajabu za Kurani Tukufu, ambazo kwazo inaitwa ni muujiza, zimeelezwa katika Sura Al-Baqara, Aali-'Imraan, An-Nisaa, Al-Maaida, Al-An'aam, Al-A'raaf, Al-Anfaal, At-Tauba, Yunus, Huud, Ar-Ra'd, Ibraahim, Al-Hijr, Al-Waaqi'ah, An-Naml, Al-Hajj, Al-Bayyina na Al-Mujadala. Kwa mfano hizi ni aya chache, Mwenyezi Mungu Anasema:

يَّهۡدِىۡ بِهِ اللّٰهُ مَنِ اتَّبَعَ رِضۡوَانَهٗ سُبُلَ السَّلٰمِ وَ يُخۡرِجُهُمۡ مِّنَ الظُّلُمٰتِ اِلَى النُّوۡرِ۔[1] شِفَآءٌ لِّمَا فِى الصُّدُوۡرِ۔[2] اَنۡزَلَ مِنَ السَّمَآءِ مَآءً فَاَحۡيَا بِهِ الۡاَرۡضَ بَعۡدَ مَوۡتِهَا۔[3] اَنۡزَلَ مِنَ السَّمَآءِ مَآءً فَسَالَتۡ اَوۡدِيَةٌ ۢ بِقَدَرِهَا۔[4] اَنۡزَلَ مِنَ السَّمَآءِ مَآءً ۡ فَتُصۡبِحُ الۡاَرۡضُ مُخۡضَرَّةً۔[5] تَقۡشَعِرُّ مِنۡهُ جُلُوۡدُ الَّذِيۡنَ يَخۡشَوۡنَ رَبَّهُمۡ ۚ ثُمَّ تَلِيۡنُ جُلُوۡدُهُمۡ وَ قُلُوۡبُهُمۡ اِلٰى ذِكۡرِ اللّٰهِ۔[6] اَلَا بِذِكۡرِ اللّٰهِ تَطۡمَئِنُّ الۡقُلُوۡبُ۔[7] اُولٰٓئِكَ كَتَبَ فِىۡ قُلُوۡبِهِمُ الۡاِيۡمَانَ وَ اَيَّدَهُمۡ بِرُوۡحٍ مِّنۡهُ۔[8] قُلۡ نَزَّلَهٗ رُوۡحُ الۡقُدُسِ مِنۡ رَّبِّكَ بِالۡحَقِّ لِيُثَبِّتَ الَّذِيۡنَ اٰمَنُوۡا وَ هُدًى وَّ بُشۡرٰى لِلۡمُسۡلِمِيۡنَ۔[9] اِنَّا نَحۡنُ نَزَّلۡنَا الذِّكۡرَ وَ اِنَّا لَهٗ لَحٰفِظُوۡنَ۔[10] فِيۡهَا كُتُبٌ قَيِّمَةٌ۔[11] قُلۡ لَّئِنِ اجۡتَمَعَتِ الۡاِنۡسُ وَ الۡجِنُّ عَلٰٓى اَنۡ يَّاۡتُوۡا بِمِثۡلِ هٰذَا الۡقُرۡاٰنِ لَا يَاۡتُوۡنَ بِمِثۡلِهٖ وَ لَوۡ كَانَ بَعۡضُهُمۡ لِبَعۡضٍ ظَهِيۡرًا۔[12]

[1] Al-Maa'da 5:17 [2] Yuunus 10:58 [3] An-Nahl 16:66 [4] Ar-Ra'd 13:18 [5] Al-Hajj 22:64 [6] Az-Zumar 39:24 [7] Ar-Ra'd 13:29 [8] Al-Mujadala 58:23 [9] An-Nahl 16:103 [10] Al-Hijr 15:10 [11] Al-Bayyina 98:4 [12] Banii Israaiil 17:89.

ikiteremka nyoyoni inaonyesha mabadiliko makubwa sana. Wanaendelea kuhuika kwayo wafu wa muda mrefu, na waliozaliwa vipofu na wakaendelea kuwa vipofu vizazi hata vizazi wanafumbua macho yao; na magonjwa ya aina aina ya ukafiri yanaendelea kuponywa; wakoma wa chuki wanatakasika. Kwayo yapatikana nuru na giza laondoka, na mwungano na Mwenyezi Mungu hupatikana na alama zake huzalika.

---

Yaani, kutokana na Kurani mwongozo wa njia za usalama unapatikana, na watu hutolewa gizani kupelekwa kwenye Nuru. Na inatibu kila ugonjwa wa kiroho. Inaponya kila ungojwa wa ndani. Mungu Ameteremsha maji ambayo kwayo ardhi iliyokufa inahuika. Ameteremsha maji yaliyotiririka katika kila bonde sawa na nafasi yake. Ameteremsha maji ambayo kwayo ardhi kame imekuwa chanikwiti. Kwayo husisimka ngozi za wamchao Mungu, kisha ngozi zao na mioyo yao hulainika kwa kumkumbuka Mungu. Kumbukeni kwa Kurani Tukufu nyoyo zinatulia. Wanaofuata Kurani Tukufu waandikiwa imani nyoyoni mwao, na hupata roho takatifu. Roho takatifu ndiye aliyeteremsha Kurani, ili Kurani iziimarishe nyoyo za Waaminio, na iwe ni mwongozo na alama ya habari njema kwa Waislamu. Sisi ndio Tulioiteremsha Kurani na sisi ndio Tuilindao. Yaani, kidhahiri na kisifa itabaki daima katika hali yake ya asili, na itakuwa chini ya hifadhi ya Mwenyezi Mungu. Tena Akasema, ndani ya Kurani Tukufu mna maarifa na kweli zote zinazopatikana kwenye Vitabu vya Mungu. Na hakuna mtu au jini awezaye kutengeneza mfano wake, hata wakisaidiana wenyewe kwa wenyewe.

Sasa, kwa nini mnaomba ishara ya adhabu na mauti kwa kuiacha ishara hii ya rehemu itoayo uzima wa milele? Kisha Akasema: "Kaumu hii inaomba adhabu ije haraka", haitaki kufaidika na ishara ya rehema. Uwaambie, kama ishara za adhabu zisingekuwa zimehusika na nyakati maalumu, basi ishara zile za adhabu zingeshateremka tayari; na adhabu haina budi kutokea, na itatokea katika wakati wasiokuwa na habari yake.

Sasa, angalieni kwa uadilifu! Wapi ndani ya aya hii kuwa miujiza imekanushwa? Aya hizo zasema kwa sauti ya juu kwamba makafiri waliomba miujiza ya maagamizi na adhabu. Basi, kwanza wakaambiwa, tazameni ipo ndani yenu ishara itoayo uzima, yaani Kurani, ambayo kwa kuwateremkieni haitaki kuwaangamizeni, bali inatoa uzima wa milele; lakini itakapowashukieni ishara ya adhabu itawaangamizeni. Kwa nini sasa mnatamani kufa bure? Na kama mnataka tu adhabu basi kumbukeni hiyo pia itakuja haraka. Basi, Mwenyezi Mungu Mtukufu Ameahidi katika aya hizi ishara ya adhabu, na Amezielekeza ishara za rehema zilizomo ndani ya Kurani Tukufu na zinazoonyesha athari yake ya ajabu zikiteremkia nyoyoni. Kwa hiyo, dhana ya mpinzani kwamba katika aya hii *la* ya kanusho inadokeza kukanusha miujiza yenyewe, inayokanusha miujiza ya aina yote, inatokana na kutokufahamu sintaksi na mofolojia. Ikumbukwe 'kanusho' athari yake inakuwa

mpaka pale anapokusudia msemaji, palipoelezwa kwa uwazi au kwa dokezo. Mathalan, mtu akisema, 'Sasa baridi imekwisha kabisa' ni dhahiri kwamba huyo amesema kuhusu eneo lake, ingawa hakutaja jina la mji wake, lakini kufahamu kutokana na kauli yake kwamba baridi imetoweka hata kwenye nchi za milimani pia, na kote kote jua kali sana linapiga, na kutoa hoja yake kwamba kwa sababu neno *la* alilolitumia lapasa kuiathiri dunia nzima, si sahihi. Waabudu masanamu wa Makka walioshindwa, ambao mwishowe waliuamini utume wa Mtume[saw] na walikubali miujiza ya Mtume[saw] kuwa ni miujiza ya kweli, nao katika zama za ukafiri hawakuwa makafiri tu, bali wakienda Roma na Irani wakaeneza kuwa Mtume[saw] yu mchawi, kwa kushangazwa naye, japo kwa njia zisizo sawa, lakini walikuwa wanakiri kutokea ishara, ambao ikirari zao zipo katika Kurani Tukufu. Wao katika kauli zao dhaifu na zisizo na nguvu ambazo zilififia mbele ya nuru kali ya unabii wa Muhammad[saw], wangewezaje kutumia *la* ya kukanusha? Kama wangekuwa wamekataa katakata, walisilimuje mwishowe kwa yakini ya hali ya juu waliyoithibitisha kwa kumwaga damu zao na kutoa uhai wao? Na maneno yao ya mara kwa mara ya siku za ukafiri wao yaliyoelezwa ndani ya Kurani Tukufu ndiyo haya haya kwamba kwa sababu ya kudanganyika na ukosefu wa busara walikuwa wanamwita Mtume[saw] mchawi — kama

Asemavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu: وَ اِنۡ یَّرَوۡا اٰیَۃً یُّعۡرِضُوۡا وَ یَقُوۡلُوۡا سِحۡرٌ مُّسۡتَمِرٌّ[23] . Yaani, wakiona ishara hugeuza uso na kusema kwa hakika huu ni uchawi hasa. Kisha, sehemu nyingine Anasema: وَ عَجِبُوۡۤا اَنۡ جَآءَهُمۡ مُّنۡذِرٌ مِّنۡهُمۡ ۫ وَ قَالَ الۡکٰفِرُوۡنَ هٰذَا سٰحِرٌ کَذَّابٌ[24]. Yaani, walistaajabu kwamba ametumwa kwao mtu mmoja kutoka miongoni mwao, na makafiri wakasema, huyu ni mchawi kadhabu. Sasa, ni dhahiri kwamba walipokuwa wakimwita Mtume[saw] kuwa mchawi kwa kuziona ishara, na tena baadaye walizikubali pia ishara hizo kuwa miujiza, na kisiwa kizima kikisilimu kikawa shahidi kwa moyo wote kwa kudumu juu ya ukweli wa miujiza mitukufu ya Mtume[saw], basi inawezekanaje kwamba hawa watu wangekataa waziwazi miujiza kwa ujumla, na katika kukataa miujiza wangetumia *la* ya kanusho iliyokuwa kinyume na ushupavu wao na rai yao ya kila siku; bali ipo dhahiri kama jua kwa viashirio kwamba popote ulipoelezwa upinzani wa makafiri ndani ya Kurani Tukufu kwamba kwa nini haikumteremkia Mtume huyu[saw] ishara yoyote, papo hapo imebainishwa kuwa hao walimaanisha kuwa kwa nini ishara miongoni mwa zile ishara tunazoziomba haiteremki.[25]

---

[23] Al-Qamar 54:3

[24] Saad 38:5

[25] Ibainike kwamba katika Kurani Tukufu siyo sehemu moja au mbili yalipoelezwa maombi ya makafiri kuonyesha ishara bali

Sasa, kwa ufupi ni kwamba umepanua sana *la* ya kanusho ya aya iliyotajwa hapo juu zaidi ya mpaka wa karina. *La* ya kanusho ya namna hii Waarabu watakuwa

---

katika sehemu kadha liimeelezwa ombi hili hili. Kwa kuziangalia sehemu hizo zote kwa pamoja inathibitika kwamba makafiri wa Makka walikuwa wanamuomba Mtume[saw] ishara za aina tatu.

(1) Zile ishara za adhabu walizoziomba makafiri wa Makka sawa na matakwa yao.

(2) Pili, zile ishara ambazo kwa sura ya adhabu au sura ya utangulizi wa adhabu ziliteremshwa juu ya nyimati zilizopita.

(3) Tatu, zile ishara ambazo kwazo pazia la ghaibu lipate kuondolewa kabisa, ambalo kuondolewa hilo ni kinyume na kuamini ghaibu. Basi masawali yaliyoulizwa kuhusu kudhihiri ishara za adhabu yamejibiwa katika Kurani Tukufu ndiyo kwamba ngojeni tu! bila shaka adhabu itashuka. Naam, imekataliwa kushusha adhabu iliyoishakadhibishwa zamani, hata hivyo imeahidiwa kuteremka adhabu ambayo ilitimia hatimaye kwa njia ya vita. Lakini kuonyesha ishara ya aina ya tatu imekataliwa kabisa; na ni dhahiri kwamba jibu la swali hili lilikuwa kukataa kabisa si vingenevyo. Kwani makafiri wakasema hatutoamini mpaka tuone ishara hii kwamba ngazi iwekwe kutoka ardhini hadi mbinguni, nawe upande mbinguni kutoka ardhini kwa ngazi hiyo, tukiwa tunashuhudia, nasi hata hivyo hatutokubali katu kupanda kwako mbinguni pekee mpaka ulete kitabu kutoka mbinguni ambacho tukisome, na tusome pia kwa kushika mikononi mwetu. Au ufanye hivi kwamba shida ya maji inayokuwepo siku zote katika mji wa Makka, itiririke mito humo kama nchi za Siria na Iraki. Na

hawajaota hata ndotoni. Nyoyo zao zilikuwa zimejaa ukweli wa Islam, ndiyo maana wote wakasilimu mwishoe, isipokuwa wachache tu walioadhibiwa

---

mababu zetu wote waliokufa toka mwanzo wa dunia mpaka leo warudi kwa kufufuka akiwemo bwana Kusayy bin Kilab, kwani mzee huyu siku zote alikuwa anasema ukweli. Tutamuuliza madai yako ni sahihi au hapana? Ishara hizi walizokuwa wakiziomba, zilikuwa zimebuniwa nao, tena si hivyo tu bali kwa kuweka masharti yaliyoelezwa ndani ya Kurani Tukufu katika sehemu mbalimbali. Basi, kwa mwenye kutafakari, madai ya Waarabu washari ni dalili iliyo wazi na bayana juu ya miujiza iliyo dhahiri, ishara wadhiha na ya ukweli wa Unabii wa Seyidna na Maulana Mtume[saw]. Mwenyezi Mungu Anajua namna zilivyowadhikisha hao vipofu kiroho nuru za ukweli wa Seyidna na Maulana Muhammad[saw] mteule, na misaada gani ya kimbingu na baraka zilikuwa zanyesha kama mvua ambazo kwa kutiwa kiwi nazo na kuzikwepa na kuzikimbia walikuwa wanaleta maombi kama hayo yasiyofaa. Ni dhahiri kwamba kuonyesha miujiza ya aina hii ni kinyume na kuamini mambo ya ghaibu. Ingawaje Mwenyezi Mungu Anao uwezo wa kuweka ngazi kutoka ardhini kwenda mpaka mbinguni ambayo watu wote wapate kuishuhudia, na kuhuisha wafu, sio elfu mbili tatu tu bali hata milioni mbili tatu ya wafu na kuwafanya washuhudie ukweli wa Mtume[saw] mbele ya wazao wao. Yote hayo Yuaweza kufanya, lakini tafakarini kidogo kufichua huku kikamilifu, imani kwa mambo ya ghaibu inapotea isababishayo thawabu na ujira, na dunia inakuwa mfano wa Kiama. Basi, kama katika

walivyoahidiwa. Na ikumbukwe kwamba *la* ya kanusho kama hii inapatikana katika kauli ya Hadhrat Masih[as] pia, nayo ni hii: Mafarisayo walimuomba Masihi[as] miujiza, yeye akavuta 'Ah' akasema: Mbona kizazi hiki chatafuta ishara? Nawaambieni kikweli kweli, kizazi hiki hakitapewa ishara. (Marko 8:11)[1]

Sasa tazama namna Masihi[as] alivyokataa katakata. Kama ukitafakari, basi upinzani wako si kitu ukilinganishwa na upinzani huu. Kwani, wewe umetoa kanusho la makafiri tu, nao pia si kwa ujumla, bali kuhusu miujiza maalum. Na ni dhahiri kwamba ukataaji wa mpinzani hauwi wenye kuaminika kikamilifu, kwani adui pengine anasema kinyume na uhakika. Lakini, Yesu anakataa mwenyewe kuonyesha miujiza, na amehusisha kutoonyesha miujiza na zama zile, kwani anasema: Nawaambieni kizazi hiki hakitapewa ishara yoyote.

---

Kiama kilicho ni wakati wa kufichua kikamilifu, imani haitafaa kitu, vivyo hivyo kuamini kwa kufichulika huku kikamilifu hakufaidishi kitu, bali imani huitwa imani hadi panapobaki uficho kidogo; yaondolewapo mapazia yote, basi hapabaki imani kuwa imani. Ndiyo sababu manabii wote walionyesha miujiza kwa kuzingatia sharti la imani juu ya ghaibu. Hakuna nabii ambaye akihuisha mji mzima akawafanya watoe ushahidi wa ukweli wa unabii wake, au kwa kuweka ngazi iendayo hadi mbinguni na kuipanda mbele ya watu wote aionyeshe tamasha dunia nzima.

---

[1]Hii kwa hakika ni Marko 8:11-12. Mwenezi

Basi kauli ipi inaweza kuwa wazi zaidi kuliko hii katika kukataa miujiza, na *la* ipi ya kanusho itakuwa wazi zaidi ya hiyo *la* ya kanusho.

Halafu tafsiri ya aya nyingine imetolewa. Na akaipinga kwa kuitenganisha na aya za nyuma na mbele. Lakini, kila mwadilifu mwenye busara anaweza kuelewa akichunguza kwa makini aya yenyewe na zingine ziihusuzo kwamba hamna hata neno moja ndani ya aya linalothibitisha kukataa miujiza, bali maneno yote yanabainisha kwamba bila shaka miujiza ilitokea. Basi, aya ile ni hii pamoja na aya nyingine husika:

وَ اِنْ مِّنْ قَرْيَةٍ اِلَّا نَحْنُ مُهْلِكُوْهَا قَبْلَ يَوْمِ الْقِيٰمَةِ اَوْ مُعَذِّبُوْهَا عَذَابًا شَدِيْدًا ؕ كَانَ ذٰلِكَ فِى الْكِتٰبِ مَسْطُوْرًا۔ وَ مَا مَنَعَنَاۤ اَنْ نُّرْسِلَ بِالْاٰيٰتِ اِلَّاۤ اَنْ كَذَّبَ بِهَا الْاَوَّلُوْنَ ؕ وَ اٰتَيْنَا ثَمُوْدَ النَّاقَةَ مُبْصِرَةً فَظَلَمُوْا بِهَا ؕ وَ مَا نُرْسِلُ بِالْاٰيٰتِ اِلَّا تَخْوِيْفًا[26] . Mwenyezi Mtukufu Anasema: Ingawa Sisi ndio Tutauangamiza kila mji kabla ya Kiama au kuuteremshia adhabu kali — hayo ndiyo yameandikwa Kitabuni — lakini kwa wakati huu Hatutumi baadhi ya zile ishara za zamani za adhabu (zilizoziangukia nyimati zilizopita kwa sura ya adhabu) kwani watu wa nyimati zilizopita walishazikadhibisha. Nasi Tuliwapa Wathamudi ishara ya ngamia jike iliyokuwa utangulizi wa adhabu ambayo ilikuwa ishara ya kudhihirisha haki (waliomdhulumu, yaani yule ngamia jike ambaye kwa sababu ya ulaji wake wa kupindukia na unywaji wake wa

[26] Banii Israaiil 17:59-60

kupita kiasi, hakukubakia maji ya kunywa bwawani n.k. kwa wakazi wa Hijr, wala hakukubakia malisho kwa wanyama wao, na walikuwa wamepatwa na taabu kubwa, huzuni na balaa). Na kusudio Letu la kuteremsha ishara za adhabu linakuwa ili watu waziogope; yaani ishara za adhabu zaonyeshwa kwa kuogofya tu. Basi, kuna faida gani ya kuomba ishara walizokadhibisha watu wa zamani walipoziona, wala hawakuogopa wala kuhofia hata kidogo kwa kuziona!

Ibainike kwamba ishara huwa za aina mbili:

(1) Ishara za kuogofya na kuadhibu zinazoweza kuitwa ishara za ghadhabu.

(2) Ishara za habari njema na tulizo ziwezazo kuitwa ishara za rehema pia.

Ishara za kuogofya huonyeshwa kwa ajili ya makafiri wakali, wenye mioyo iliyopindamana, waasi, wasio na imani na wenye tabia za Kifirauni ili waogope, na nyoyo zao zishikwe na hofu ya ghadhabu na hasira ya Mwenyezi Mungu. Na ishara za habari njema hudhihirika kwa ajili ya watakao haki, waaminio waliohalisika, watafutao ukweli ambao kwa unyenyekevu na upole wa nyoyo zao wanataka kupta yakini kamili na kujiongezea imani. Ishara za habari njema hazikusudii kuogofya na kutisha, bali kusudio lake huwa kutuliza waja wake watii na kustawisha hali

zao za imani na yakini, na kutuliza nyoyo zao zisumbukazo. Hivyo, mwaminio kwa njia ya Kurani Tukufu daima huendelea kupata ishara za habari njema, na kuongezeka imani na yakini. Muumini anapata utulivu kwa ishara za habari njema, na ule wasiwasi uliopo ndani ya mwanadamu kiasili unatoweka, na amani inateremka moyoni. Mwaminio kwa kufuata Kitabu cha Allah huendelea kupata ishara za habari njema mpaka siku ya mwisho ya maisha yake, na ishara zipatiazo utulivu na raha huendelea kumteremkia ili adumu kupata maendeleo mengi yasiyokoma katika maarifa na yakini na kufikia ***Hakkul-Yakiin*** [haki yenye yakini]. Furaha nyingine inayopatikana kwa bishara za habari njema ni kwamba kama mwaminio anavyozidi kupata maendeleo katika maarifa na nguvu ya imani, ndivyo hivyo asongavyo mbele katika huba na mapenzi ya Mungu siku hadi siku kwa sababu ya kushuhudia neema, baraka na hisani za dhahiri na za batini, zilizo wazi na za siri, za Mwenyezi Mungu, zijaazo ishara za habari njema. Basi, kwa hakika ishara za bishara njema huwa zenye athari kubwa zaidi na baraka na zifikishazo kwenye kusudio hasa, zimwasilishazo msafiri wa kiroho kwenye daraja ya maarifa kamili na mapenzi ya dhati ya Mwenyezi Mungu, ambayo ndiyo ya mwisho kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu. Na ishara za habari njema zimetajwa sana ndani ya Kurani Tukufu hata

kwamba haijaziwekea kikomo, bali imetoa ahadi ya kudumu kwamba wafuasi wa kweli wa Kurani Tukufu wataendelea daima dawamu kupata ishara hizi, kama Anavyosema: لَهُمُ الْبُشْرٰى فِى الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَ فِى الْاٰخِرَةِ ؕ لَا تَبْدِيْلَ لِكَلِمٰتِ اللّٰهِ ؕ ذٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيْمُ[27]. Yaani, waaminio wataendelea kupata ishara za habari njema katika maisha ya dunia na Akhera, ambazo wataendelea kupata kwazo maendeleo yasio na kikomo katika nyanja za maarifa na mapenzi duniani na akhera. Hayo ndiyo maneno ya Mwenyezi Mungu ambayo hayatatoweka kamwe, na kupata ishara za bishara njema ndio ufaulu mkubwa (yaani, hili ndilo jambo linalofikisha kwenye kilele cha mapenzi na maarifa ya Mwenyezi Mungu).

Sasa, yapasa kufahamu kwamba katika aya aliyotoa mpinzani ili kuleta upinzani, Mwenyezi Mungu Ameeleza ishara za kuogofya tu, kama inavyodhihirika katika aya: وَ مَا نُرْسِلُ بِالْاٰيٰتِ اِلَّا تَخْوِيْفًا[28]. Kwani, kwa kuzichukulia ishara zote za Mwenyezi Mungu kuwa za adhabu tu, aya hii ikifasiriwa hivi kwamba Sisi Hutoa ishara zote kwa shabaha tu ya kuogofya pasipokuwa na sababu nyingine yoyote iwayo, maana hizi zitakuwa batili kwa uwazi kabisa. Kama ilivyokwishaelezwa hivi punde, ishara

[27] Yuunus 10:65

[28] Na Hatuzipeleki ishara ila kwa kuhadharisha (Banii Israaiil 17:60).

zinatolewa kwa shabaha mbili, ama kwa kuogopesha au kutoa habari njema. Kurani Tukufu na Biblia zabainisha bishara za aina hizi mbili sehemu mbalimbali. Basi kwa kuwa ishara ni za aina mbili, hivyo neno اَلْاٰیَات lililopo katika aya hiyo hapo juu (ambayo maana yake ni zile ishara) kwa vyovyote litakuwa linamaanisha tu kwamba ishara hizo zilizo ndani ya uwezo wa Mungu ni ishara za kuogofya tu, ilhali kufahamu ishara zote ni za kuogofya tu pekee ni kinyume na uhakika — jambo ambalo haliwezi kuwa sahihi kulingana na Kitabu cha Allah, wala akili, wala dhamiri ya mwenye moyo safi.

Sasa, kwa kuwa imeshathibitika waziwazi kwamba katika aya zilizo hapo juu, ishara za kuogofya tu zimetajwa miongoni mwa aina mbili za ishara, basi jambo lililobaki kuamuliiwa ni kwamba je aya hii (iliyo وَ مَا مَنَعَنَا hadi mwisho) itakuwa na maana kwamba Mwenyezi Mungu Hakuonyesha ishara za adhabu mkononi mwa Mtume[saw], au ichukuliwe maana hii kwamba hazikuonyeshwa zile ishara miongoni mwa ishara za adhabu zilizoonyeshwa kwa nyimati za zamani, au je maana hii ya tatu ni muhimu kuzingatiwa kwamba miujiza ya aina zote mbili ya kuogofya ilikuwa imeendelea kuonyeshwa na Mtume[saw] isipokuwa baadhi ya miujiza mahususi ambayo nyimati za zamani zilizikadhibisha kwa kufahamu hiyo haikuwa ni miujiza?

Ibainike, basi kwamba kwa kuziangalia aya zinazobishaniwa inadhahirika waziwazi kuwa maana ya kwanza na ya pili, kwa vyovyote haziko sahihi. Kwani, kuchukulia maana ya aya hiyo hapo juu kwamba zile ishara za kuogofya za kila anwai Tunazoweza kuonyesha, na ishara zote za kuadhibu za nyuma zaidi Tunazoweza kuzionyesha bila kikomo, Hatukuonyesha, kwa sababu nyimati zilizopita zilizikadhibisha; maana hizi ni batili kabisa. Kwani ni dhahiri kwamba watu wa nyimati za zamani walikadhibisha bishara zile walizozishuhudia wao; sababu yake ni kwamba kwa kukadhibisha ni lazima kitu kinachokadhibishwa kiwe kinashuhudiwa. Ishara ambayo haijashuhudiwa itakadhibishwaje? Kwani, miongoni mwa ishara zisizoshuhudiwa zipo ishara za daraja ya juu katika uwezo wa Allah, ambazo mtu yeyote asiweze kuzikadhibisha, na shingo zote ziiname kwazo, kwani Mwenyezi Mungu Ana uwezo wa kuonyesha kila aina ya ishara. Tena kwa kuwa ishara za nguvu za Mwenyezi Mungu hazina mpaka wala hazina kikomo, yawezekanaje kuwa sahihi kusema kwamba ishara zote hizo zilishuhudiwa ndani ya muda mfupi na zikakadhibishwa pia. Bila shaka ndani ya muda mfupi kitashuhudiwa kitu kilicho na kikomo. Kwa vyovyote, maana hii tu ndiyo itakuwa sahihi ya aya hii kwamba baadhi ya zile bishara walizokuwa wameshashuhudia

makafiri wa zamani na walikwishazikadhibisha, kuzituma tena ikaonelewa kuwa bure, kama karina pia inavyoongoza kwenye maana hii. Yaani sehemu hii, habari ya ngamia jike wa Wathamudi Aliyotaja Mwenyezi Mungu ni karina kubwa juu ya jambo hili kuwa sehemu hii habari ya ishara za zamani na zilizokataliwa imetajwa, zilizokuwa miongoni mwa ishara za kuogofya. Na hii ndiyo maana ya tatu ambayo ndiyo sawa na sahihi.

Tena hapa jambo jingine lapasa kuzingatiwa na waadilifu, ambalo itadhihirika kwalo kwamba kwa aya وَ مَا مَنَعَنَآ اَنْ نُّرْسِلَ بِالْاٰيٰتِ[29] inathibitika kutokea miujiza siyo kukanusha miujiza. Kwani kiambishi awali *al* cha neno الآيات, sawa na kanuni ya sintaksia hakiwezi kukosa sura mbili; ama itakuwa na maana ya aina zote au aina mahususi. Kama inayo maana ya aina zote, basi itafasiriwa kwamba hakuna kilichotuzuia Sisi kupeleka miujiza ya kila aina ila watu wa zamani kuzikadhibisha; na kama itakuwa na maana ya aina maalum, basi maana yake itakuwa ni kwamba hakuna kilichotuzuia Sisi kutuma ishara mahususi (makafiri wanayoomba) isipokuwa kwamba ishara hizo walizikadhibisha watu wa zamani. Kwa vyovyote vile kwa maana hizi zote

[29] Na hakuna kingetuzuia kuzipeleka Ishara ila ya kwamba watu wa zamani walizikadhibisha.

mbili kutokea kwa miujiza kunathibitika. Kwani, ikiwa maana ndiyo hii kwamba Hatukupeleka ishara zote kwa sababu ya ukadhibishaji wa watu wa zamani, basi inathibitika kwayo kupelekwa baadhi ya ishara; mathalan mtu akisema 'Mimi sikumpa Zaid mali yangu yote', basi inathibitika wazi kwayo kwamba bila shaka yeye amempa Zaidi sehemu fulani ya mali yake. Na kama tuchukue maana hii kwamba Hatukutuma baadhi ya ishara mahsusi, pia inathibitika kutumwa kwa miujiza ya aina nyingine. Mathalani, kama mtu akisema: 'Mimi sikumpa Zaid baadhi ya vitu mahususi', itabainika wazi kwayo kuwa baadhi ya vitu vingine lazima amempa. Kwa vyovyote, kama mtu akiangalia aya za mbele na za nyuma za aya hii namna zinavyoeleza, kwa jiha zote mbili habari ya ishara za adhabu, na kisha aangalie mara nyingine na kutafakari kuwa je ni sahihi maana hii na inaweza kukubalika ya kwamba ishara zote na maajabu ya Mwenyezi Mungu yatokanayo mara kwa mara na kudra Yake isiyo na kikomo na yasio na mipaka, watu wa zamani walizikadhibisha katika zama zao zilizo na kikomo. Tena afikirie mara ya tatu kwa jicho lenye uadilifu kwamba je hapa pametajwa ishara mahususi za kuogofya au pametajwa ishara za habari njema na rehema pia? Kisha mara ya nne aitupie jicho ال ya الآيات kwamba yatoa maana gani? Basi baada ya kuangalia kwa namna hizi nne, kila mtu, ila yule tu aliyepo mbali na

kupenda haki kutokana na chuki, atapata ndani mwake sio ushahidi mmoja tu bali atapata maelfu ya ushahidi kwamba sehemu hiyo kanusho limetumika kwa kanusho la aina moja mahususi tu ya ishara, lisilohusiana na aina nyingine, bali kinyume chake yathibitika kwa hizo lazima zilitokea. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu Anabainisha wazi katika aya hizi kwamba wakati huu ishara za kuogofya wanazoziomba hawa watu hazikutumwa kwa sababu nyimati za zamani zimekwishazikadhibisha. Hivyo, ishara zilizokadhibishwa hapo awali, kuziteremsha tena ni dalili ya udhaifu na mbali na shani ya Mwenye kudura zisizo na kikomo. Basi katika aya hizi mna dokezo hili kwa uwazi kwamba ishara za adhabu lazima zitateremka lakini kwa namna nyingine. Kuna haja gani ya kuonyesha ishara zile zile za Hadhrat Musa[as] au ishara zile zile za Hadhrat Nuhu[as] na za watu wa Luti, Waadi na Wathamudi? Basi, maelezo zaidi ya aya hizi yametolewa hasa katika aya zingine, kama vile Allah Mtukufu Anavyosema:

وَإِن يَرَوْا كُلَّ آيَةٍ لَّا يُؤْمِنُوا بِهَا ۖ حَتَّىٰ إِذَا جَاءُوكَ يُجَادِلُونَكَ[30] وَإِذَا جَاءَتْهُمْ آيَةٌ قَالُوا لَن نُّؤْمِنَ حَتَّىٰ نُؤْتَىٰ
مِثْلَ مَا أُوتِيَ رُسُلُ اللَّهِ ۘ اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ[31] قُلْ إِنِّي عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّي وَكَذَّبْتُم بِهِ ۚ مَا عِندِي
مَا تَسْتَعْجِلُونَ بِهِ ۚ إِنِ الْحُكْمُ إِلَّا لِلَّهِ ۖ يَقُصُّ الْحَقَّ ۖ وَهُوَ خَيْرُ الْفَاصِلِينَ[32] قَدْ جَاءَكُم بَصَائِرُ مِن رَّبِّكُمْ ۖ فَمَنْ

---

30 Al-An'aam 6:26

31 Al-An'aam 6:125

32 Al-An'aam 6:58

أَبْصَرَ فَلِنَفْسِهِ ۖ وَمَنْ عَمِيَ فَعَلَيْهَا ۚ وَمَا أَنَا عَلَيْكُمْ بِحَفِيظٍ[33] وَيَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ[34] قُلْ هُوَ الْقَادِرُ عَلَىٰ أَنْ
يَبْعَثَ عَلَيْكُمْ عَذَابًا مِنْ فَوْقِكُمْ أَوْ مِنْ تَحْتِ أَرْجُلِكُمْ أَوْ يَلْبِسَكُمْ شِيَعًا وَيُذِيقَ بَعْضَكُمْ بَأْسَ بَعْضٍ[35] وَقُلِ
الْحَمْدُ لِلَّهِ سَيُرِيكُمْ آيَاتِهِ فَتَعْرِفُونَهَا[36] قُلْ لَكُمْ مِيعَادُ يَوْمٍ لَا تَسْتَأْخِرُونَ عَنْهُ سَاعَةً وَلَا تَسْتَقْدِمُونَ[37] وَ
يَسْتَنْبِئُونَكَ أَحَقٌّ هُوَ ۖ قُلْ إِي وَرَبِّي إِنَّهُ لَحَقٌّ ۖ وَمَا أَنْتُمْ بِمُعْجِزِينَ[38] سَنُرِيهِمْ آيَاتِنَا فِي الْآفَاقِ وَفِي
أَنْفُسِهِمْ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُ الْحَقُّ[39] خُلِقَ الْإِنْسَانُ مِنْ عَجَلٍ ۚ سَأُورِيكُمْ آيَاتِي فَلَا تَسْتَعْجِلُونِ[40]

Yaani: Watu hawa hawaamini kwa kuona ishara zote, kisha wanapokuja kwako wanabishana nawe, na waonapo ishara yoyote husema, sisi hatutoiamini kamwe mpaka tupewe na sisi yale waliyopewa Mitume. Sema nimekuja na uthibitisho kamili kutoka kwa Mola wangu, nanyi mnauona uthibitisho huu kisha mwaukadhibisha. Ile mnayoiharakia kuomba (yaani adhabu) haiko mkononi wangu. Kutoa amri ya mwisho ndiyo madaraka ya Mwenyezi Mungu pekee, Yeye ndiye Ataibainisha haki, Naye ndiye Mbora wa mahakimu

---

33 Al-An'aam 6:105

34 Al-Hajj 22:48

35 Al-An'aam 6:66

36 An-Naml 27:94

37 Sabaa' 34:31

38 Yuunus 10:54

39 Haa Miim 41:54

40 Al-Anbiyaa 21:38

Ambaye Atatoa hukumu baina yangu na yenu. Mungu Amekupatieni ishara zing'aazo kuhusu utume wangu, basi atakayezitambua ndiye amejinufaisha nafsi yake na atakayepofuka, hasara yake itakuwa juu yake, nami si mlinzi juu yenu. Na wanakuomba adhabu itoke haraka. Waambie Muumba Huyo Anao uwezo wa kuwateremshieni adhabu kutoka juu yenu au kutoka chini ya miguu yenu, au Akitaka, kwa kuwagawa ninyi katika makundi mawili Alionjeshe kundi moja adhabu ya mapigano ya kundi jingine. Na sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu. Si muda mrefu Mwenyezi Mungu Atawaonyesheni ishara mtakazozitambua. Na sema, miadi kwa ajili yenu ni mwaka mmoja kamili[41], hamtaweza kuiahirisha wala kuitanguliza. Na wanakuuliza, je hili ni jambo la kweli? Sema, naam naapa kwa jina la Mola wangu kwamba ni kweli, nanyi hamwezi kumzuia Mwenyezi Mungu kuzitimiza ahadi Zake. Muda si mrefu Tutawaonyesha ishara Zetu pembeni mwa nchi yao na ndani mwao pia, mpaka watabainikiwa kwamba huyu ni Nabii mkweli. Mwanadamu asili yake ni

---

[41] *Yaum* muradi wake hapa ni mwaka. Katika Biblia pia matumizi kama haya yanapatikana. Basi, baada ya mwaka mzima barabara watu wa Makka walishukiwa adhabu ya vita ya Badri, iliyokuwa ni vita ya kwanza.

yenye haraka. Karibu Nitakuonesheni Mimi ishara Zangu, kwa hiyo msinihimize.

Sasa, angalia namna zilivyotolewa katika aya hizi ahadi wazi na imara za kuonyesha ishara zilizoombwa hata ikasemwa kwamba zitaonyeshwa ishara bayana kabisa kiasi hiki kwamba mtazitambua. Sasa, mtu akisema kwamba hii tumekubali kuwa katika Kurani Tukufu sehemu nyingi zimetolewa ahadi za ishara za adhabu kuwa lazima ishara hizi zitaonyeshwa siku fulani, na pia tumekubali kwamba ahadi hizi zote zilitimia katika zama Mwenyezi Mungu Alipowaondolea Waislamu udhaifu na unyonge kwa kudhihirisha kudura Yake, na kufikisha idadi yao ndogo hadi maelfu, na kwa njia yao Akawaangamiza makafiri wote waliokuwa wakiomba ishara za adhabu huko Makka katika zama za uasi wao na dhuluma na ukatili kwa kiburi cha hali ya juu sana. Lakini sehemu gani katika Kurani Tukufu upo uhakikisho kwamba Mtume[saw] alionyesha ishara nyingine mbali na ishara hizi? Ibainike kwamba habari ya kuonyesha ishara imo ndani ya Kurani Tukufu katika sehemu nyingi, baadhi ya sehemu imerejelea ishara zake zilizopita pia. Angalieni aya كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوْا بِهٖٓ اَوَّلَ مَرَّةٍ[42] (Juzuu 7, Sura Al-An‘aam). Baadhi ya sehemu, ikielezea tabia ya

[42] Katika hali ile ile waliyokuwa nayo walipozikataa ishara Zetu kwa mara ya kwanza. Al-An‘aam 6:111

dhuluma ya makafiri, imetaja ikrari yao ya aina hii kwamba wanasema kwa kuziona ishara kuwa huu ni uchawi tu. Angalieni aya: وَ اِنْ يَّرَوْا اٰيَةً يُّعْرِضُوْا وَ يَقُوْلُوْا سِحْرٌ مُّسْتَمِرٌّ[43] . Baadhi ya sehemu walipokiri makafiri waziwazi kuona bishara, Amewasilisha ushahidi wao, kama Asemavyo: وَ شَهِدُوْٓا اَنَّ الرَّسُوْلَ حَقٌّ وَّ جَآءَهُمُ الْبَيِّنٰتُ[44]. Yaani wao waliushuhudia ukweli wa Mtume[saw] na walifikiwa na ishara bayana. Na baadhi ya sehemu Ameeleza wazi baadhi ya miujiza, kwa mfano muujiza wa mwezi kupasuka, ulio muujiza mkubwa na ulio mfano kamili wa kudura ya Mungu. Habari zake tumezieleza kwa kirefu katika kitabu *Surma Chashme Ariya*; anayetaka kufahamu kinaganaga aweza kuona ndani yake. Sehemu hii izingatiwe pia kwamba wale watu waliokuwa wakimuomba Mtume[saw] kuonyesha ishara iliyobuniwa nao, mwishowe wakawa mashahidi pia wa ishara za Mtume[saw], kwani hao hao ndio kwa kusilimu wakaisambaza dini ya Kiislamu kwenye sehemu za Mashariki na Magharibi, na pia wakaandikisha shuhuda zao za kuona miujiza na matabiri katika vitabu vya Hadithi. Basi, katika zama hizi ipo njia ya kustaajabisha kuwa wanaendelea kuwasilisha mara kwa mara ukadhibishaji wa zama za

---

43 Na wakiona Ishara hugeuka upande na husema: Uchawi unaoendelea! Al-Qamar 54:3

44 Aali ‘Imraan 3:87

ujinga wa watukufu hao walioisha kutupilia mbali hatimaye na kutubu; lakini hawakukubali ushuhuda wao ule waliotoa baada ya kukubali njia ilionyooka. Miujiza ya Mtume[saw] inang'aa kutoka pande zote nne nazo zawezaje kufichika. Miujiza pekee iliyothibiti kwa ushahidi wa Masahaba[ra] ni elfu tatu na bishara pengine ni zaidi ya elfu kumi zilizotimia katika nyakati zao na zinaendelea kutimia. Isitoshe, baadhi ya miujiza na bishara za Kurani Tukufu ni kama zinavyoshuhudiwa na kutambulika katika zama hizi kwa ajili yetu pia na hakuna yeyote awezaye kuzikataa. Nazo ni hizi:

(1) Muujiza wa ishara ya adhabu, walioonyeshwa makafiri wa zama zile, huo kwa hakika kwa ajili yetu pia ni ishara inayofaa kusemwa kuwa imeshuhudiwa na kuhisiwa. Kwani haya ni matokeo ya lazima ya mambo yaliyotangulia asiyoweza kuyakataa katu yeyote anayeafikiana na anayehitilafiana. Kwanza jambo hili lilo msingi wa muujiza, ni dhahiri shahiri lililokubalika kuthibitika kwamba ishara hii ya adhabu iliombwa ambapo Mtume[saw] pamoja na Masahaba zake wachache walikuwa wanaudhiwa na kuteswa kule Makka kwa sababu ya kuwaita watu kwenye haki. Na siku hizo zilikuwa siku za udhaifu na unyonge kwa dini ya Kiislamu kiasi hiki kwamba makafiri wakiwadhihaki na kuwacheka Waislamu walikuwa wanawaambia: Kama ninyi mpo juu ya haki, kwa nini mwaadhibiwa na

kuteswa, kusumbuliwa na kutaabishwa kwa mikono yetu? Na mbona huyo Mungu wenu mnayemtegemea Hawasaidieni, na kwa nini m kundi dogo mno ambalo si muda mrefu litaangamia? Na kama ninyi m wakweli, mbona hatuteremkiwi adhabu? Yale yote yaliosemwa ndani ya sehemu mbalimbali za Kurani Tukufu kwa kuwajibu makafiri katika zama za dhiki na mateso ni jambo la pili lililotangulia muujiza huo ili kuelewa shani adhimu ya utabiri huo. Kwani zama zile zilikuwa za hatari kwa Mtume[saw] na Masahaba zake kiasi hiki kwamba kila wakati walihofia usalama wa maisha yao, na ushinde ulionekana kutoka pande nne zote. Basi katika wakati huo makafiri walipoomba ishara za adhabu, waliambiwa kwa uwazi kabisa kwamba si muda mrefu mtaonyeshwa ishara za ushindi wa Islam na ya kuadhibiwa kwenu. Na Islam ambayo kwa sasa inaonekana kama mbegu tu, siku moja itajidhihirisha kama mti mkubwa, na wale wanaoomba ishara za adhabu watakuja kuuawa kwa upanga, na kisiwa chote cha Arabu kitakuja safishwa na kufuru na makafiri, na utawala wa bara lote la Arabu utakuja kuangukia mikononi mwa waaminio. Na Mwenyezi Mungu Ataiimarisha dini ya Islam katika bara Arabu kiasi hiki kwamba ibada ya masanamu haitatokea tena, na hali ya sasa iliyo ya hofu, itakuja badilika kabisa kuwa hali ya amani, na Islam itapata nguvu zaidi na itaendelea kupata ushindi kiasi kwamba

itatandaza kivuli cha nusura na ushindi wake utaenea sehemu za mbali na utaasisiwa ufalme mkubwa ambao hautaondoka mpaka mwisho wa dunia.

Sasa, mtu akielewa kwanza kwa kuangalia mambo hayo mawili yaliyotangulia muujiza huo kwamba zama bishara hii ilipotolewa zilikuwa ni zama za dhiki, ushinde na misiba kwa Islam, na utabiri uliotolewa ulikuwa kinyume kabisa na hali ya sasa na mbali na kufikirika na kuwazwa, bali ulionekana kabisa miongoni mwa muhali wa kawaida, kisha baadaye aitupie jicho la uadilifu historia ya dini ya Kiislamu iliyomo mkononi mwa maadui na marafiki, kwamba namna bishara hii ilivyotimia barabara, na jinsi ilivyoathiri nyoyo kwa namna ya kuogofya na kudhihiri kwa nguvu zote nchi za mashariki na magharibi, basi kwa yakini na bila shaka atauita utabiri huu, muujiza ulioshuhudiwa kwa macho, ambamo ndani yake hatakuwa na shaka hata sawa na chembe.

Halafu muujiza wa pili wa Kurani Tukufu ulio kama twashuhudia na kuuhisi, ni yale mabadiliko ya ajabu yaliyodhihiri katika Masahaba[ra] wa Mtume Mtukufu[saw] kwa baraka ya kuifuata Kurani Tukufu na kwa athari ya usuhuba wa Mtume[saw]. Tunapoona kwamba hawa watu walikuwa na desturi na tabia gani kabla hawajasilimu, na kisha baada ya usuhuba wa Mtume[saw] na kwa kuifuata Kurani Tukufu wakawa namna gani, na namna gani walihama hali mbovu za hulka, itikadi, mienendo, uneni,

mwenendo, vitendo na mazoea yao yote kwenye hali taibu na takatifu, twalazimika kukiri kwa kuona athari hiyo adhimu iliyowajalia hao wenye kutu, upya wa ajabu, nuru na mng'aro kwamba mageuzi haya kwa hakika yalikuwa mageuzi ya kimuujiza ambayo yaliletwa na mkono wa Mwenyezi Mungu hasa. Mwenyezi Mungu ndani ya Kurani Tukufu Anasema: Niliwakuta kuwa wafu Nikawafufua, na Niliwaona wakiwa karibu kuanguka shimoni mwa Jahanamu, Nikawaokoa katika hali hiyo ya kutisha. Niliwakuta wakiwa wagonjwa, Nikawaponya. Niliwakuta gizani, Nikawajalia nuru. Kwa kuonyesha muujiza huu, Mwenyezi Mungu Mtukufu Ameelezea upande mmoja hali mbaya za Waarabu walizokuwa nazo kabla ya kukubali Uislamu, na kwa upande wa pili Ameeleza hali zao za utakaso walizopata baada ya kusilimu, ili mtu akiangalia hali yao ya awali ilivyokuwa katika zama za ukafiri, na kisha asome hali yao iliyodhihiri baada ya kujiunga na Islam, basi kwa kuhabarishika na matukio ya aina zote mbili, atafahamu kwa yakini kamili kwamba mapinduzi haya ni mapinduzi yasiyo ya kawaida, ambayo yapaswa kuitwa muujiza.

Kisha, muujiza wa tatu wa Kurani Tukufu ulio mbele ya macho yetu, una kweli zake, maarifa yake, elimu zake nyepesi na nukta zake vilivyojaa ndani ya ibara zake zenye balagha na ufasaha. Muujiza huu umeelezwa kwa kutiliwa mkazo sana katika Kurani Tukufu, na imesema

kwamba hata kama majini na watu wote wajumuike kuleta mfano wake hawataweza. Muujiza huu unathibitika na kuhakikishika kutoka dalili hii kwamba hadi zama hizi ambapo inapita zaidi ya miaka elfu moja na mia tatu, ijapokuwa Kurani Tukufu inanadi katika kila kona duniani na inatoa wito kwa kupaza sauti wa هَلْ مِنْ مُّعَارِضٍ[45] lakini kamwe hakuna aliyeitikia. Basi, hii yathibitisha kwa uwazi kwamba nguvu zote za kibinadam hazina uwezo wa kukabiliana na kushindana na Kurani Tukufu; bali kama kwa kutolea uzuri mmoja tu miongoni mwa mazuri mamia ya Kurani Tukufu ikiombwa kuleta mfano wake, itashindikana kwa binadamu aliye dhaifu kuleta mfano wa sehemu yake hiyo moja tu. Kwa mfano, uzuri mmojawapo wa Kurani Tukufu ni huu pia kwamba imejikusanyia maarifa yote ya kidini. Hakuna ukweli wowote wa kidini unaohusiana na haki na hekima, ambao haupatikani ndani ya Kurani Tukufu. Lakini yu nani atuonyeshe kitabu kingine kilicho na sifa hii ndani yake? Kama mtu ana shaka kuhusu Kurani Tukufu kujikusanyia uzuri wote wa dini basi mwenye wasiwasi kama huyu akiwa ni Mkristo, Mwaria, Mbarhamu au mkanamungu yuaweza kujiridhisha kwa kutahini namna apendavyo, nasi twachukua jukumu la kumridhisha, sharti atujie mtafuta

[45] Je yupo mshindani yeyote.

haki. Kweli zote takatifu zilizomo katika Biblia au mambo ya haki na ya hekima yaliyomo ndani ya vitabu vya wenye busara ambayo tumepata kuyaona, au baadhi ya kweli zilizopata kuandikika kwa bahati tu katika Veda ya Mabaniani au zilizobakia humo ambazo tumeziona au nukta za hekima na maarifa zilizomo ndani ya mamia ya vitabu vya masufii tulizopata kuzijua, hizo zote tunazikuta ndani ya Kurani Tukufu. Na kwa tajiriba kamili tuliyo nayo tangu miaka thelathini kwa mtazamo wa kina na kamili, tumebainikiwa kwa yakinifu kamili kwamba hakuna ukweli wowote wa kiroho unaoathiri ukamilishaji wa nafsi, na ulezi wa nguvu za akili na roho usiopata kuelezwa ndani ya Kurani Tukufu. Huu sio uzoefu wetu tu bali pia ni madai ya Kurani Tukufu, ambayo si mimi tu bali maelfu ya wanazuoni wameendelea kuyajaribu tangu mwanzo na wameendelea kushuhudia ukweli wake.

Kisha, muujiza wa nne wa Kurani Tukufu ni athari zake za kiroho zinazodumu kuhifadhiwa ndani yake. Yaani, wanaoifuata wanafikia daraja za kukubaliwa na Mwenyezi Mungu na wanajaliwa neema ya kuzungumza na Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Husikia maombi yao na kuwajibu kwa upendo na rehema Yake, na Huwajulisha baadhi ya siri za ghaibu kama Manabii, na Huwapambanua baina ya viumbe wengine kwa ishara ya msaada na nusura Yake. Na hii pia ni ishara

itakayodumu mpaka siku ya Kiama katika umati wa Mtume Muhammad[saw] na toka zamani imedumu kudhihirika na hata sasa ipo na imethibitika kuwepo. Miongoni mwa Waislamu, wapo mpaka leo hii watu wa namna hii ambao Mwenyezi Mungu Akiwajalia msaada Wake hasa, Huwaenzi kwa funuo za kweli, ndoto njema, na habari za ghaibu.

Sasa, Enyi watafuta ukweli, wenye njaa na kiu ya kupata ishara za kweli! Hebu angalieni kwa uadilifu na tafakarini kwa nia njema kwamba ishara Alizotaja Mwenyezi Mungu ndani ya Kurani Tukufu ni ishara za daraja ya juu kiasi gani, na namna gani zashuhudiwa na kuhisiwa katika kila zama. Haikubaki hata alama ya miujiza ya Manabii wa zamani. Ni visa tu, Mungu Anajua usahihi wao ukoje. Hususani ukweli wa miujiza ya Hadhrat Isa[as] iliyoandikwa ndani ya Injili, licha ya kuwa katika sura ya visa na hadithi na kutiliwa chumvi nyingi, shaka na wasiwasi unaizingira kiasi hiki kwamba inakuwa vigumu kuuondelea mbali. Hata tukichukulia kwamba yale yote yaliyoandikwa ndani ya Injili kuhusiana na Hadhrat Masih[as] kuwa wagonjwa kama vilema na viwete, waliopooza, vipofu n.k. walikuwa wanapona kwa yeye kuwagusa tu, na kwamba maelezo haya hayajapigwa chuku, na yachukuliwe kidhahiri kama yalivyo, na hayana maana nyingine zaidi ya hiyo, hata hivyo hauthibitiki ubora wowote wa Hadhrat Masihi[as]

kwa mambo haya. Kwanza, katika siku hizo kulikuwepo na bwawa la maji alimoingia wakati mahususi mwenye maradhi kama hayo, akaondolewa maradhi yote mara moja, kama vile ilivyoelezwa ndani ya Injili yenyewe. Isitoshe, imethibitika kupitia uchunguzi na utafiti wa muda mrefu kwamba ubingwa wa kuponya maradhi ni tawi moja la elimu miongoni mwa matawi ya elimu, ambayo mabingwa wake wengi wapo mpaka sasa, ambamo mnahitaji mazoezi ya kuelekeza moyo vikali na kutumia nguvu za ubongo na kuathiri kudhibiti mawazo. Hivyo, elimu hii haihusiani na unabii hata kidogo bali pia haimhitaji mtu kuwa mwema. Elimu hii imekuwa imezoeleka toka zamani hadi sasa. Miongoni mwa Waislamu kuna baadhi ya wanazuoni wakubwa kama vile Muhyiddin Ibn Arabii, mwandishi wa kitabu cha *Fusuus* na baadhi ya wanazuoni wa *Nakshbandi* waliokuwa mabingwa wa kazi hii, hivi kwamba katika zama zao haukuwepo mfano wao. Kuhusu baadhi yao yasemwa kwamba kwa umakini kamili waliweza kuzungumza na watu waliokufa muda mchache kabla kwa idhini ya Mwenyezi Mungu [46], na kuwaponya

[46] Siyo kinyume na kanuni ya asili kufufuka kwa mtu aliyekufa muda mchache, kwa dakika chache au saa chache kupitia elimu hiyo. Tunapoona kwa macho yetu sisi wenyewe kwamba mara baada ya kufa baadhi ya wanyama wanahuika kwa dawa fulani,

wagonjwa mia mbili au miatatu kwa kuwakalisha kulia na kushoto, kwa mtazamo mmoja tu. Na baadhi yao wasiokuwa na uzoefu mkubwa wakamponya mgonjwa kwa kumgusa au kwa kugusa nguo yake. Katika mazoezi haya, mfanyaji wakati wa kufanya anahisi kana kwamba nguvu fulani inatoka ndani mwake wakati wa kumwathiri mgonjwa na pengine hata mgonjwa anashuhudia pia kuwa ndani mwake sumu ikisogea inaendelea kuteremka kuelekea viungo vyake vya chini hadi kupotea kabisa. Kuhusu elimu hii vipo vitabu vingi, nami nafikiri hata katika Wahindu pia vitakuwepo vitabu vya elimu hii. Fani ya kiini macho iliyoletwa hivi karibuni na Waingireza kwa hakika pia ni tawi moja la elimu hiyo. Kwa kuchunguza Injili inabainika kwamba Yesu pia alikuwa na mazoezi ya elimu hii kiasi fulani ingawa hakuwa mkamilifu. Watu wa zama zile walikuwa na uelewa mdogo sana na hawakuwa na habari ya elimu hii, kwa hiyo amali hii ilisifiwa sana kupita mipaka yake. Lakini kadiri ulivyoendelea kudhirika uhakika wake kwa mpito wa wakati, watu waliendelea kupungukiwa itikadi yao kubwa hata kwamba wengine walitoa rai hii kuwa kazi ya kuwaponya wagonjwa kwa mazoezi ya namna hii au kuwatibu vichaa haina ubora wowote, bali haina

---

basi kwa nini ni vigumu na mbali na kufikirika, kwa binadamu kuhuika. Mwandishi

ulazima wa kuwa mwaminifu, licha ya kuwa iwe ni dalili ya Unabii au ya Uwalii. Kauli yao pia ni kwamba mazoezi marefu ya kuwaponya wagonjwa wa kimwili, na kuendelea kuyashughulikia hayo usiku na mchana yanadhuru maendeleo ya kiroho. Na kazi ya malezi ya kiroho inafanyika kidogo sana na mtu kama huyo, na nguvu iangazayo ya moyo wake inatindika mno. Yaweza kufikiriwa kuwa ndiyo sababu Hadhrat Masihi[as] alikuwa dhaifu sana katika malezi ya kiroho, kama ambavyo Padre Taylor anayeonekana mtu maarufu kwa sababu ya cheo chake na pia kwa sababu ya ustadi wake binafsi, anaandika kwa masikitiko sana kwamba: Malezi ya kiroho ya Masihi[as] yathibitika kuwa dhaifu, na watu waliosuhubiana naye waitwao wanafunzi wake hawakuweza kuonyesha mfano wowote bora wa ulezi wa kiroho wala ukamilifu wa nguvu za kibinadamu. (Laiti Masih[as] angalijielekeza kidogo tu kwenye shuguli dhahiri ya kuyaponya magonjwa na badala yake angejielekeza zaidi kwenye kutibu udhaifu wa kiroho wa wanafunzi wake hususani Yuda Iskariote). Hapa Padre huyo anasema haya pia: Kama malezi ya kiroho ya wanafunzi wa Yesu na uimara katika imani vikilinganishwa na ya masahaba wa Mtume Mwarabu[saw], twalazimika kukiri kwa masikitiko kwamba wanafunzi wa Hadhrat Masih[as] hawakuimarika na walikuwa nyuma kabisa wala usuhuba wa Hadhrat Masih[as] haukupanua

nguvu za akili zao na moyo kiasi kwamba wangeweza kusifiwa wakilinganishwa na masahaba wa Mtume Mtukufu[saw]; bali kwenye kila hatua ulikuwa unathibitika uoga, itikadi pungufu, ufinyu wa moyo, upendo wa dunia na usaliti. Lakini kwa masahaba wa Mtume[saw] unyofu na uaminifu uliodhihirika ni vigumu mfano wake kupatikana ndani ya wafuasi wa nabii mwingine yeyote. Basi athari hii ilitokana na malezi ya kiroho yaliyofanywa kikamilifu, ambayo yaliwafikisha toka chini hadi kileleni kwa kuwabadilisha kabisa. Kadhalika Waingireza wanazuoni wengi wameandika vitabu ambamo wamekiri kwamba kama tuone hali ya Mtume Mwarabu[saw] ya kumwelekea Mungu, na kumtegemea, uimara wa kibinafsi, mafundisho makamilifu na yatakasayo, kutia athari, kuwarekebisha watu wengi miongoni mwa walioharibika, na misaada ya dhahiri na batini ya Mwenyezi Mungu, hata kwa kutenga na ile miujiza, vilivyoandikwa kuhusu yeye, hata hivyo uadilifu wetu unatulazimisha kukiri kwamba mambo haya yote yaliyodhihirika kwake, hayo pia ni fauka ya kawaida na yako nje ya nguvu ya mwanadamu na ni alama ya kutosha kabisa kwa kutambua unabii sahihi na wakweli. Hakuna mwanadamu awezaye kufanikiwa katika mambo yote haya wala hawezi kupata misaada kama hiyo ya ghaibu Asipokuwa Mwenyezi Mungu pamoja naye.

## Jibu la Swali la Tatu

Mawazo aliyotoa huyu Mkristo kwenye ibara yake kwa sura ya upinzani, kwa hakika sio upinzani bali ni fahamu tatu potofu zilizoibuka moyoni mwake kutokana na upungufu wa uchunguzi. Hapa chini tunaondoa fahamu hizi potofu.

Kuhusu fahamu potofu ya kwanza jawabu ni hili kwamba alama ya nabii mkweli siyo kabisa hii kwamba yeye pia awe na elimu kama Mungu ya kila jambo kwa kudumu lilofichika; bali kuwa na elimu ya ghaibu kwa nguvu Yake binafsi na sifa Yake binafsi ni sifa hasa ya Mwenyezi Mungu pekee. Toka kale waja wa Mungu wana itikadi kuhusu Yule Asiyeumbwa kuwa binafsi na elimu ya ghaibu, na wana imani kuhusu viumbe vyote vingine kutostahiki kibinafsi na ya uwezekano wa kujaliwa tu na Mwenyezi Mungu pekee — yaani, itikadi hii kwamba ni lazima kwa Dhati ya Mwenyezi Mungu kuwa na elimu ya ghaibu na ni sifa binafsi ya Dhati Yake Tukufu kwamba Awe Mjuzi wa ghaibu; lakini, haijuzu kwa viumbe wote wenye sifa ya kuangamia na wasio na uhakika, kushirikiana na Mwenyezi Mungu katika sifa hii na vile vile katika sifa zingine. Kama ambavyo haiwezekani kuwa mshirika wa Mwenyezi Mungu katika Dhati Yake, ndivyo hivyo isivyowezekana kuhusiana na sifa Zake. Hivyo basi, haiwezekani kwa viumbe kuwa na sifa ya kujua elimu ya ghaibu kibinafsi,

bila kujali wao ni Manabii au Muhadathina au Mawalii. Naam, kujua elimu ya siri za ghaibu kupitia ufunuo, wameendelea kupata hadhi yake waja mahususi na wateule, na hata sasa wanaipata, ambayo tunaikuta kwa wafuasi wa Mtume[saw] tu na si kwa mwingine yeyote. Hii ndiyo kawaida ya Mwenyezi Mungu inayoendelea kwamba mara moja moja Huwahabarisha waja Wake mahususi baadhi ya siri Zake maalum, na wananyunyiziwa neema ya elimu ya ghaibu kwa wakati maalum na uliokadiriwa. Kwa hakika waliowekwa karibu na Mwenyezi Mungu hujaribiwa kwayo ukamilifu wao na kutambuliwa, kwamba baadhi ya wakati mambo yaliyofichikana ya mustakabali au siri zilizofichika wanajulishwa, lakini siyo kwa hiari yao na matakwa na mamlaka yao wenyewe, bali neema hizi zote wanapewa kwa matakwa, hiari na mamlaka ya Mwenyezi Mungu.

Kawaida ya Yule Aliye Kheri tupu kwa wale wanaofuata radhi Yake na huwa wake na kujipoteza ndani Yake, ni kwamba mara nyingi Husikiliza maombi yao, na saa nyingine Huwadhihirishia kitendo chake cha zamani au utashi Wake wa siku zijazo. Lakini hawapati kujua chochote bila kujulishwa na Mwenyezi Mungu. Ingawaje wanakuwa wamewekwa karibu na Mwenyezi Mungu lakini hawawi Mungu, wanafahamu wafahamishwapo, wanajua wanapojulishwa, wanaona waonyeshwapo, husema wafanywapo kusema, na

hawawi kitu binafsi. Nguvu kuu Inapowafunulia kusema husema, Iwaonyeshwapo huona, Iwasikilizishapo husikia. Na maadamu Mwenyezi Mungu Hajawadhihirishia jambo lilofichika wanakuwa hawana habari ya jambo hilo. Ushahidi wake unapatikana katika maisha ya Manabii wote. Angalieni namna Hadhrat Masihi[as] asemavyo akikiri kutojua kwake kwamba habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala mwana, ila Baba (Marko 13:32). Na kisha anasema kwamba sifanyi neno kwa nafsi yangu (yaani siwezi kufanya chochote), ila kama Baba Alivyonifundisha ndivyo ninenavyo[47], sina uwezo wa kumnyanyua yeyote daraja ya juu ya ucha Mungu. Kwa nini kuniita mwema? Hakuna aliye mwema ila Mmoja, ndiye Mungu.[48]

Ilmuradi, hakuna Nabii aliyedai kuwa na mamlaka au mjuzi wa mambo ya ghaibu. Hebu mtazameni mja mnyenyekevu huyu anayeitwa Masihi, na ambaye majahili waabudu viumbe wanamchukulia kuwa Mungu, namna alivyodhihirisha kila sehemu kwa kauli na vitendo vyake kwamba yu mtu dhaifu na mnyonge na ndani yake hamna uzuri wowote binafsi. Na ikrari ya mwisho ambayo juu yake hatima yake ikatokea i kwa

[47] Yohana 8:28

[48] Marko 10:18

maneno ya kupendeza sana. Basi imeandikwa katika Injili hivi kwamba yeye yaani Masihi (akisikia habari ya kukamatwa kwake) alifadhaika na kuhuzunika mno akasema kuwaambia (yaani, wanafunzi wake) kwamba nafsi yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa. Na akienda mbele kidogo akaanguka chini (yaani akasujudu), na akaomba dua, ikiwezekana, saa hii iniepuke; na akasema, Ee Aba, Ee Baba, kila kitu kinawezekana kwako; niondolee kikombe hiki[49]. Yaani, U Mwenye uwezo juu ya kila kitu na mimi ni mtu dhaifu na mnyonge. Ukiondoa balaa hii, yaweza kuondoka. Na hatimaye akatoa roho yake akisema: *Eloi, Eloi, lama sabakthani,* ambayo tafsiri yake ni hii: Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?[50]

Angalieni, sasa, japo dua haikupokelewa kwa sababu ilikuwa *Takdiri Mubram* [Takdiri isiyotanguka], kiumbe masikini alikuwa na uwezo gani mbele ya uamuzi wa mkataa wa Muumba! Lakini Hadhrat Masihi alifikisha ikrari ya unyonge na unyenyekevu wake kileleni kwa kutarajia kukubalika. Kama angalijua kwamba dua yake itakataliwa, haitakubaliwa katu, kwa nini angeendelea kuomba dua ya kugombolewa kwake usiku kucha

49 Mathayo 26:38-39

50 Mathayo 27:46

mpaka alfajiri, na kwa nini angejitia nafsi yake kwa msisitizo na wanafunzi wake katika shida isiyofaa?

Basi sawa na kauli ya bwana mpinzani kulikuwa moyoni mwake Yesu kwamba Mungu ndiye Anajua hatima, si mimi. Kisha kutotimia kwa baadhi ya bishara za Hadhrat Masihi[as] pia kwa hakika kulikuwa kwa sababu tu ya kutojua siri zilizofichika, alikuwa anakosea katika kuzisherehi, kama alivyosema: Katika ulimwengu mpya, atakapoketi mwana wa Adamu katika kiti cha utukufu wake, ninyi nanyi mtaketi katika viti kumi na viwili (enyi wanafunzi wangu kumi na wawili). Angalieni Mathayo 20:28.[51]

Lakini kutoka kwenye Injili hiyo hiyo inabainika kwamba Yuda Iskariote hakubahatika kupata kiti hicho. Akasikia habari ya kukalia kiti cha ufalme, lakini hakupata bahati ya kukalia kiti cha ufalme. Sasa, swali lazuka kwa unyofu na ukweli kwamba kama Hadhrat Masihi angekuwa na habari ya kuritadi kwa mtu huyo na mwisho wake mbaya, kwa nini angepasha habari njema ya uongo ya kukalia kiti cha ufalme? Kadhalika safari moja yeye kwa kuona mtini mmoja kutoka mbali aliuendea kwa hamu ya kula tini, lakini alipoufikia akagundua hauna hata tini moja, akakasirika sana, akiwa katika hali ya hasira akaulaani mtini, lakini haikudhihiri

[51] Hili ni kosa la maandishi, sahihi ni Mathayo 19:28. Mwenezi

athari yake mbaya kwenye mtini. Kama angelikuwa anajua mambo ya ghaibu angekusudiaje kwenda kula matunda ya mti usiokuwa na matunda?

Vile vile safari moja mwanamke mmoja aligusa nguo yake; yeye akaanza kuuliza kila upande nani kaigusa nguo yangu? Kama angejua elimu ya ghaibu isingekuwa taabu kumjua aliyegusa nguo yake. Na safari moja alitabiri pia kwamba watu wa zama hizo hawatakufa mpaka yatokee haya yote (yaani ujio wa Masihi kwa mara ya pili na kuanguka kwa nyota n.k.). Lakini ni dhahiri shahiri kwamba katika zama zile hakuna nyota yoyote ya mbinguni iliyoanguka ardhini wala Yesu hakuja duniani kuhukumu, achilia mbali karne ile, karne kumi na nane zingine zimepita juu yake, na hata karne ya kumi na tisa inakaribia kuisha. Shuhuda hizi chache zinatosha kuthibitisha Yesu kutojua mambo ya ghaibu, ambazo hazitokani na kitabu kingine bali tumeziandika kwa kuona kutoka katika Injili nne. Hii hii ndiyo hali ya Manabii wengine pia wa Kiisraeli. Yakobo alikuwa Nabii, lakini hakujua kilichokuwa kinatokea kwa mwanaye jangwani mwa kijiji hicho hicho. Nabii Daniel mpaka pale Mwenyezi Mungu Alipomfunulia uaguzi wa ndoto ya Nebukadnezar hakujua ndoto ikoje na uaguzi wake ukoje?

Basi kutokana na uchunguzi huu wote imebainika kuwa kauli hii ya Nabii anaposema kwamba jambo hili

Mwenyezi Mungu ndiye Anajua, mimi silijui ndiyo sahihi na yalingana na mahala pake na ndiyo heshima kwa Nabii huyo, na ni fakhari ya uabudiwaji wake. Bali kwa maneno kama haya heshima yake yazidi machoni pa Bwana wake Karimu, siyo kwamba Unabii unapata dosari kidogo. Naam, kama yatakiwa kufanya utafiti huu kwamba siri za ghaibu zinazopatikana kwa kujulishwa na Mwenyezi Mungu, Mtume[saw] alizipata hizo kiasi gani, basi mimi niko tayari kutoa uthibitisho mmoja mkubwa ili kuhakikisha kwamba bishara za Mtume[saw] ni nyingi mara elfu zaidi kwa idadi na kwa ubora kuliko bishara zote za manabii ziliotajwa ndani ya Torati na Injili na ndani ya Bibilia nzima, zinazojulikana kutoka katika Hadithi za Mtume[saw] zilizoandikwa kwa kufanya uchunguzi mkubwa. Maelezo yake kwa ufupi lakini ya kutosha na ya kuridhisha na yenye kuathiri sana yanapatikana ndani ya Kurani Tukufu. Kisha, Waislamu hawanavyo visa tu mkononi mwao kama wafuasi wa dini nyingine, bali katika kila karne wamekuwa wakiwaambia wafuasi wa dini nyingine, hata sasa wanawaambia kwamba baraka hizi zote zipo kwa kudumu ndani ya Islam. Enyi ndugu! njooni mkajaribu kwanza kisha mkubali. Lakini, hakuna asikiaye wito huu. Hoja ya Mwenyezi Mungu imekamilika juu yao kwamba tunawaita waje, hawaji; tunawaonyesha, hawaoni.

Wameyageuza macho na masikio kutoka kwetu wasije wakasikia na kuona na kupata mwongozo.

Fahamu potofu ya pili, aliyotoa mpizani — yaani hii ya kwamba maelezo ya Kurani Tukufu kuhusu idadi ya As-habul-Kahfi [watu wa Pango] siyo sahihi — ni madai tu matupu. Mpinzani hakuandika chochote kwa nini maelezo hayo si sahihi; na kuali ipi ni sahihi, na ni dalili zipi za kuonyesha usahihi wake, ili dalili zake zichunguzwe na majibu ya kutosheleza yatolewe. Ikiwa mpinzani alikuwa na walakini kidogo kuhusu maelezo ya Kurani Tukufu ilimpasa kutoa sababu zake. Haimfai mtafuta ukweli kusema 'si sahihi' pasipo kutoa sababu zake.

Fahamu potofu ya tatu iliyozalika moyoni mwa mpinzani ni huu kwamba imeandikwa ndani ya Kurani Tukufu kuwa mfalme fulani (ambaye utalii wake umetajwa ndani ya Kurani Tukufu) alifikia sehemu fulani akifanya matembezi, alipoona jua likizama katika dimbwi la matope. Sasa Mkristo huyu kwa kuchukua tamathali kuwa tafsiri sisisi aleta shutuma eti jua ni kubwa mno lilituaje ndani ya dimbwi dogo la matope? Hii ndiyo kama mtu aseme kwamba ndani ya Injili Masihi ameitwa kuwa mwanakondoo wa Mungu; hii yawezekanaje? Kwani, mwanakondoo ndiye anayekuwa na pembe kichwani, na manyoya mwilini na anayetembea akiinamisha kichwa chini kama wanyama wenye miguu minne, na anayevila wanavyovila? Ee

bwana! Umesikia wapi na kwa nani kwamba Kurani Tukufu imedai jua kutua kwa hakika kwenye dimbwi la matope? Kurani Tukufu ikieleza mawazo ya mtu huyo, inasema jua likaonekana kwake kutua matopeni. Basi, hii ndiyo hali ya uonaji wa mtu, iliyoelezwa kwamba yeye alifika sehemu ambapo jua halikuonekana likitua nyuma ya mlima au makazi ya watu au miti, kama ilivyo desturi, bali lilionekana kuzama dimbwini mwa matope. Muradi wake ni kwamba hapakuwa na makao wala miti wala milima karibu, wala hapakuwa na dalili yoyote ya vitu hivi kwa kadiri ya macho yalivyoweza kuona, bali kulikuwa na dimbwi la matope tu ambamo jua lilionekana linatua.

Angalieni muktadha wa aya kwa makini, je kuna simulizi yoyote ya utafiti wa kitaalamu mahali hapo? Pametajwa tu matembezi ya mtu mmoja ya masafa marefu. Shabaha yake ndiyo kuthibitisha kwamba huyo alifika mahali pa ukiwa. Kwa hiyo, kuihusisha sehemu hii na masuala ya elimu ya nyota, haifai kabisa. Mathalan, kama mtu akisema leo usiku anga lilikuwa wazi, halikuwa na mawingu na nyota zilionekana ziking'aa kama nukta za mbingu, hapo tukianza kubishana tukisema je nyota ziko ndogo kama nukta, na kutoa vitabu kuhusu elimu ya nyota, bila shaka kitendo hiki kitakuwa ni kama cha majahili tu. Kwani, mzungumzaji hakukusudia kueleza jambo lenyewe lilivyo, bali

aliongelea kiistiara kama waongeavyo watu wote. Enyi watu mnaoinywa damu ya Yesu na kuula mwili katika Ekaristi Takatifu hadi sasa hamjapata habari ya mafumbo na stiara? Wote wanajua kwamba katika mazungumzo ya kawaida ya kila nchi mlango mpana upo wazi wa kutumia mafumbo na stiara. Na wahyi wa Mwenyezi Mungu nao hutumia mafumbo na stiara zile zile ambazo watu wanazitumia kwa urahisi katika mazungumzo na maongezi yao ya kila siku. Siyo desturi ya wahyi wa Mungu kufuata kila sehemu na kila mahali istilahi ngumu za falsafa, kwani wanaoambiwa ni watu wa kawaida. Basi yalazimu mazungumzu yafanyike kulingana na ufahamu wao na misemo yao. Ni sawa kueleza hakika na maarifa mepesi, lakini haifai kuachana na misemo na kujitenga kabisa na tashbihi na stiara za kawaida, kwa mtu ambaye jukumu lake ni kuongea na watu wa kawaida sawa na njia yao ili waelewe kauli yake na nyoyo zao zipate kuathirika. Hivyo, imekubalika kwamba hakuna kitabu kilichofunuliwa ambamo yameachiliwa mbali matumizi ya tashbihi na istiara au imejuzu kujitenga nayo. Je limewahi kuja duniani Neno lolote la Mungu la namna hii? Kama tukitafakari, tutaona kwamba sisi wenyewe katika maongezi yetu ya kila siku tunatumia mamia ya tashbihi na istiara, na hakuna anayepinga. Kwa mfano, inasemwa hilali ni nyembamba kama unywele au nyota ni kama nukta au

mwezi umejificha ndani ya wingu, na jua lilichomoza tangu masaa matatu bado limepanda juu kiasi cha mkuki tu, au tumekula sahani ya pilau, au tumekunywa kikombe cha sharubati. Kwa kusikia maneno haya hamna yeyote ashtukaye kwamba hilali inawezaje kuwa nyembamba kama unywele, au kwa sababu gani nyota zinaweza kuwa ndogo kiasi cha nukta, au mwezi unawezaje kuingia kwenye wingu, au inawezekanaje jua linalopita kwa kasi likifunika maelfu ya maili kwa siku liende ndani ya saa tatu masafa mafupi kiasi cha urefu wa mkuki tu. Pia kwa kula sahani ya pilau au kunywa kikombe cha sharubati hakuna yeyote anayeweza kuwaza kwamba eti sahani na kikombe pia akavimeza kwa kuvunja vipande vipande! Bali watafahamu kwamba pilau na maji vilivyomo ndani yao ameila na kuyanywa. Hata mpinzani mwenye akili hapendi kulipinga jambo lilolo wazi kabisa. Nimewahi kusikia kutoka kwa Wakristo wenye kupenda uadilifu kwamba watu wanaouleta upinzani wa namna hii miongoni mwetu ni wale tu ambao ama ni majahili sana au ni wenye chuki kali.

Je hii ni njia ya haki kwamba kauli yoyote ikiwemo katika Neno la Mungu kwa sura ya mfano au istiara, basi kauli hii ipingwe kwa kuchukuliwa kuwa hakika halisi? Kama ndivyo hivyo, basi hakitasalimika kupingwa Kitabu chochote kilichofunuliwa dhidi ya shutuma hizi.

Wanaosafiri baharini kwa meli au kwa stima, huona kila siku tamasha hili kwamba jua lachomoza kutoka kwenye maji na kuzama ndani ya maji; na mara nyingi huambizana wao kwa wao kulingana na wanavyoliona kuwa hili limetoka na hilo limezama. Sasa ni wazi kwamba wakati wa mazungumzo hayo kufungua mbele yao vitabu vya elimu ya nyota na kujadili mfumo wa jua [na siari zake] ni kana kwamba kujibiwa kwamba: Mjinga we! Je wewe tu unajua elimu hii, sisi hatujui?

Bwana Mkristo ameipinga Kurani Tukufu, lakini amesahau vifungu vile vya Biblia ambavyo vinapingwa kweli na kwa hakika. Mathalan, angalieni ndani ya Injili ya Mathayo na Marko imeandikwa kwamba mtamuona Masihi anateremka kutoka mbinguni kuja kuwahukumu wanaadamu pindi jua litakapotiwa giza na mwezi hautatoa mwanga wake na nyota zitaanguka mbinguni.[52] Sasa, elimu hii hii ya nyota inauleta mushkili huu kwamba inawezekanaje nyota zote zianguke juu ya ardhi na zikivunjika vipande vipande zidondoke sehemu fulani ya ardhi, na binadamu wasipate shida na taabu yoyote kwa kuzianguka na wote wabaki hai na salama ilhali kuanguka kwa nyota moja tu inatosha kwa kuwaangamiza waishao ardhi. Tena ni la kutafakariwa kwamba zitakapodondoka nyota ardhini na kufutilia

[52] Mathayo 24:29; Marko 13:24-25

mbali kabisa viumbe wote waliopo ardhini, itakuwaje kuwa sawa kauli hii ya Yesu kwamba "Mtaniona kwenye mawingu nikishuka kutoka mbinguni"? [53] Watu watakapokuwa wamekufa wakiwa wamezikwa chini ya maelfu ya nyota, nani atashuhudia kushuka kwa Yesu? Na ardhi iliyopo kwa sababu ya mvuto wa nyota itawezaje kubaki salama na katika hali yake ya kawaida? Na Masihi atawaita wateule wepi (kama ilivyoelezwa katika Injili) kutoka sehemu za mbali na atawakemea wepi na kuwaonya? Kwani, kuanguka kwa nyota lazima kutasababisha maangamizi ya vitu vyote na kifo cha wote bali kutasababisha mapinduzi ya ardhi. Hebu tazama, je maneno haya yote hayapingani na elimu ya nyota au la? Kadhalika injili inakabiliwa shutuma nyingine kwa mujibu wa elimu ya nyota, nayo ni hii ndani ya Mathayo: tazama, ile nyota waliyoiona (yaani Majusi) mashariki ikawatangulia, hata ikaenda ikasimama juu ya mahali alipokuwapo mtoto," (Mathayo 2:9).

Sasa, Wakristo watuambie, kwa mujibu wa elimu ya nyota, hii nyota ya ajabu iliyoenda pamoja na Majusi inaitwaje? Na mwendo huu uliokuwa wa aina gani na inathibitika kwa mujibu wa kanuni gani? Sijui Injili ya Mathayo kuhusu nyota kama hii inawezaje kujiepusha kukosolewa na wataalamu wa elimu ya nyota! Baadhi ya

---

[53] Mathayo 24:30; Marko 13:26

watu hujibu kwa kukerwa kwamba haya siyo maneno ya Yesu bali ni ya Mathayo, na maneno ya Mathayo sisi hatuyaamini kuwa ni maneno ya ufunuo. Ni jibu 'zuri' hili ambalo kwalo ukafichuka barabara uhakika wa Injili kuwa wa kiufunuo. Nami nasema kwamba hata kama haya siyo maneno ya Yesu bali ni ya Mathayo au mtu mwingine yeyote yule, lakini kauli ya Masihi pia (ambayo inaaminiwa kuwa ni kauli iliyofunuliwa na ambayo imepingwa nasi hivi punde) inafanana na kulingana na hii hii. Haya thibitisheni kauli yake kwamba inalingana na kanuni ya elimu ya nyota. Isitoshe, ikumbukwe kwamba hii kauli siyo ya kiufunuo bali imeingizwa na mtu ndani ya Injili, kwa nini sasa mnadai kwamba Injili zilizomo mkononi mwenu, maneno yake yote ni ya kiufunuo? Kwa nini msitangaze kwa uwazi kwamba mbali na maneno machache yaliyotoka kinywani mwa Yesu, mengine yote yaliyoandikwa ndani ya Injili, wameyaandika waandishi kulingana na fikira na akili na ufahamu wao yasiyoweza kuchukuliwa kuwa hayana makosa. Nilivyojua kutoka katika maandiko ya Mapadre, rai hii imeelezwa pia hadharani yaani imekubaliwa na wote kuhusu Injili kwamba miujiza n.k. ambayo imeelezwa katika Injili kihistoria, siyo habari ya ufunuo, bali ni waandishi wa Injili wameandika kwa vyanzo vya nje — kukisia au kwa kusikia. Kwa kifupi mapadre kwa ikrari hii wamejaribu

kujiepusha na yale mashambulizi mengi yanayofanywa dhidi ya Injili; nao wamekiri kuwa katika kila Injili takribani sehemu kumi ni za watu na sehemu moja ni maneno ya Mungu. Kwa sababu ya ikrari hizi hasara walizozipata miongoni mwao moja ni hii kuwa wamepoteza miujiza ya Masihi, hawanao tena uthibitisho wake wa kutuliza na kutosha. Kwani, ingawaje waandishi wengi wa Injili wameandika miujiza ya Masihi kihistoria ndani ya Injili kutoka kwao binafsi, lakini kauli hasa ya Masihi mwenyewe ambayo inaitwa kuwa ni ufunuo inaonekana ikihitilafiana dhahiri shahiri na kauli ya wanafunzi wake, bali ni kinyume chake na dhidi yake. Sababu yake ni kwamba Masihi katika kauli yake inayosemwa kuwa ya kiufunuo, amekataa hapa na pale kuonyesha miujiza, na amewajibu waziwazi walioomba muujiza kwamba hamtaonyeshwa muujiza wowote. Ndiyo maana Herode pia alipomuomba muujiza, yeye hakuonyesha. Na watu wengi walitaka kuona miujiza yake na pia walimwomba kuonyesha ishara lakini alikataa moja kwa moja na hakuweza kuonyesha ishara yoyote. Isitoshe, alikesha usiku mzima akimuomba Mungu ishara hii kwamba ahifadhiwe kukamatwa na Wayahudi, lakini hata ishara hii pia hakupewa na dua yake ilikataliwa. Na baada ya kutundikwa msalabani Wayahudi walisema kwa moyo wa kweli kwamba kama atashuka sasa kutoka juu ya

msalaba kwa kufufuka, sisi sote tutamuamini, lakini hakuweza kushuka pia. Basi, kwa matukio haya yote inabainika kinagaubaga kwamba kauli zilizopo za kiufunuo katika Injili, hizo zinakataa wazi kabisa kuwa Masihi alionyesha miujiza. Na kama kwa bahati lipo neno ambalo kwalo tunaweza kufikiria kuhusu Masihi kuwa mwenye miujiza, basi kwa hakika neno hilo lina maana zaidi ya moja na linaweza kuwa na tafsiri nyingi tofauti. Haionekani kulazimika kuchukua maana yake ya dhahiri, au kwa kutumia nguvu ithibitishwe kuwa alionyesha miujiza ambayo wamesimulia waandishi wa Injili wenyewe. Wala hakuna kauli yoyote iliyotamkwa na Masihi mwenyewe inayoongoza kwa uwazi kutokea na kuthibitika kwa miujiza; bali maneno hasa na yenye mkazo sana ya Masihi yanaonyesha kwamba hata muujiza mmoja haukuonyeshwa na yeye.[54] Inashangaza, kwa nini Wakristo hawayaamini na hawayategemei maneno ambayo ni maneno hasa ya Masihi na yanaitwa ya kiufunuo na yemetoka kinywani mwa Masihi? Kwa nini maneno mengine yanaaminika na kwa nini yanatiliwa mkazo zaidi ya kiasi, ambayo kwa mujibu wa

---

[54] Usadikishaji wa miujiza ya yule Masihi[as] tu umo katika Kurani Tukufu ambaye hakudai kabisa uungu, kwani kumekuwa na Masihi wengi na kutakuwa na wengine. Halafu uthibitisho wa Kurani ni wenye maana zaidi ya moja, ambao hausadikishi kauli za waandishi wa Injili. Mwandishi

ikrari ya Wakristo wenyewe hayakufunuliwa bali yameingia ndani ya Injili kama historia, na hayana uhusiano wowote na silsila ya ufunuo, na yanakinzana na ibara za ufunuo. Basi, ibara za kiufunuo na ibara zisizo za kiufunuo zikinzanapo, njia nyingine ipi inafaa kutatua tatizo hili ila hii tu kwamba ibara ambazo si za kiufunuo zisitegemewe na yasiaminiwe maneno ya waandishi wa Injili yaliyotiwa chumvi. Na kutia kwao chumvi hapa na pale ni dhahiri, kama ilivyo ile aya ya mwisho ya Injili ya Yohana ambayo kwayo Injili hiyo takatifu imemalizwa, nayo ni hii: "Kuna mambo mengi aliyoyafanya Yesu ambayo yakiandikwa moja moja, nadhani hata ulimwengu usingtosha kwa vile vitabu vitakavyoandikwa". Angalieni ilivyotiwa chumvi! Ulimwengu ukayatoshea maajabu ya ardhi na mbingu, lakini ulimgwengu hautoshei kwa maisha ya Masihi ya miaka mitatu au ya miwili na nusu. Ziaminiwe vipi riwaya za watia chumvi kama hawa!

Wahindu nao waliandika vitabu vya namna hiyo kuhusiana na ma-Autari wao, na kwa namna hii hii walijenga vizuri jengo la uzushi. Hivyo basi watu hao pia wameathirika sana na uzushi ule, na kuanzia upande huu wa nchi, mpaka upande wa mwisho wa nchi, ikapenya nyoyoni *Raam-Raam* na *Krishan-Krishan*. Jambo lenyewe ni kwamba vitabu vilivyotungwa vinavyojaa uzushi vinakuwa kama makaburi yapakwayo

sana rangi nyeupe kwa nje na kung'arishwa, lakini ndani hamna kitu. Hali ya ndani wanawezaje kujua watu hawa wasio na habari waliozaliwa mamia ya miaka baadaye, wakapewa vitabu vilivyotengenezwa tayari kwa kudhihirisha ni vyenye baraka na vilivyo safi kana kwamba vimeshuka kutoka mbinguni kwa hali na sura hiyo hiyo. Basi wanajuaje mkusanyiko huu kwa hakika jinsi gani umeandaliwa? Ni machache sana macho makali yapenyayo ndani kwa kupasua mapazia na kufahamu hakika hasa na kumkamata mwizi; na roho zinazoathirika na uchawi wa uzushi, zipo nyingi kiasi hiki kwamba ni vigumu kuzikadiria. Ndiyo sababu ulimwengu mmoja ukaangamia na unaendelea kuangamia. Wajinga hawakutafakari kabisa juu ya suala la lazima la uthibitisho au ukosefu wa uthibitisho, na hawakupenda kujihadhari na njia ya kudumu na iliyo jambo la asili la mipango na mipaka inayoendelea baina ya wanadamu tangu kale na wakajitia bure mtegoni mwa Shetani. Jinsi mualkemia mshari anavyomuahidi juha, kwa kuchukua rupia elfu kutoka kwake, kuzibadilisha kuwa dhahabu zenye thamani ya milioni moja au mbili, wadanganyifu wakapoteza imani ya kweli na safi ya wajinga na kuahidi unyofu wa uongo na baraka za uongo ambazo hazipo kivitendo na wala hazina uthibitisho wowote. Wakawafanya hatimaye kuwa wabaya zaidi kuliko wao wenyewe katika ufisadi, hila,

kupenda dunia na kufuata nafsi iamrishayo sana maovu. Mwishowe, yapasa kukumbuka kwamba ushahidi mdogo tu wa Kurani Tukufu kuhusu miujiza iliyoonyeshwa na bishara zilizotolewa na Mtume[saw] ni bora zaidi mara elifu kuliko kilima kikubwa cha Injili cha miujiza na bishara za Masihi. Ni bora, kwa nini? Kwa sababu hii hii kwamba kutokana na ikrari ya mapadre wahakiki kuwa maneno ya Injili ni maneno ya wanafunzi wenyewe, tena yasiyoshuhudiwa nao kwa macho yao wala hawakutolea mfululizo wa wasimulizi wala hawakudai wamejionea wenyewe. Lakini, chochote kilichoandikwa katika Kurani Tukufu kuhusu miujiza ya Mtume[saw] ni ushuhuda hasa uliotukuka wa Mwenyezi Mungu Mkweli, Mtukufu. Hata kama hii ingekuwa ni aya moja tu hata hivyo ingetosha kabisa, lakini alhamdu-lillahi Kurani Tukufu yote imejaa ushahidi huu. Hamna ulinganisho baina ya ushahidi uliotukuka wa Mwenyezi Mungu na shuhuda za uongo zilizotiwa chumvi zisizoonwa na macho:

به نزدیک دانائے بیدار دل    جوئے سیم بهتر زِ صد تودهٔ گِل[55]

Kwa nini yapasa kushangaa mambo ya uzushi? Mengi ya namna hii yamefanyika na yafanyika. Wakristo wenyewe wanakiri kwamba katika zama za mwanzoni, watu wengi

[55] Kwa mwenye hekima na busara, kijito cha fedha ni bora kuliko vilima mia vya udongo.

miongoni mwetu kwa kutunga vitabu wenyewe na kuandika humo mambo makubwa ya watakatifu wao halafu wamekuwa wakivinasibisha hivyo kwa Mwenyezi Mungu. Na ilikuwa inadaiwa kwamba hivyo ni vitabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu.[56] Sasa, ughushi

---

[56] Iliyomo ndani ya Injili, miujiza ya Masihi isiyojuzu, isivyothibitika, iliyotiwa chumvi au kuhusu sifa zake zisizofaa, ni vigumu kuhakiki kwamba lini na wakati gani mambo haya yaliingizwa katika Injili. Ingawa Wakristo wamekubali kwamba waandishi wa Injili wameongeza mambo haya wenyewe, lakini kwa mtazamo wangu nyongeza hizi zilifanywa hatua kwa hatua. Wazushi wajanja wamekuwa wanapata baadaye fursa ya kutosha. Naam, vitabu kadhaa vilivyozushwa ambavyo vilipata umaarufu wa kudumu kama vitabu vilivyofunuliwa, viliandikwa na kusambazwa na Wakristo na Wayahudi katika siku za mwanzo kabisa. Basi, kwa 'baraka' hii ya kughushi, si Injili moja, bali Injili nyingi zilienea. Ni kauli ya Wakristo wenyewe kwamba Injili nyingi za uzushi zilitungwa baada ya Masihi. Miongoni mwao ni Injili ya Barnabas pia. Haya ni maneno ya Wakristo wenyewe. Lakini mimi nasema kwamba kwa vile kuna hitilafu kubwa kati ya Injili hizo na Injili nne zilizozoeleka kiasi kwamba Injili ya Barnabas inakanusha kabisa kifo cha Masihi msalabani, na inakataa Utatu, na haitambui uungu na uwana wa Masihi, na kwa maneno ya wazi kabisa inatoa habari njema ya ujio wa Mtukufu Mtume[saw]. Sasa kwa nini tukubali dai hili la Wakristo lisilothibitishwa kwa dalili kwamba eti Injili walizoeneza wao ndizo za kweli, na zinazokinzana nazo ndizo za uwongo. Zaidi ya hayo, uzushi ulipokuwa umezoeleka mno miongoni mwa

ulipokuwa ni mazoea ya zamani ya Wakristo na Wayahudi, hatuoni sababu kwamba Injili ya Mathayo na nyinginezo zisihusishwe na mazoea haya, ilhali kama yule tajiri ambaye daftari lake la maelezo yake ya akunti linafichua siri zilizofichika kutokana na hitilafu na makosa yaliyo dhahiri, ndivyo hivyo ujanja ule unadhihirika kwa Injili zote nne waliotaka kuficha, ndiyo sababu wasiwasi mkubwa umezalika moyoni mwa

---

Wakristo hata kwamba baadhi ya 'walimu wakamilifu' kwa kuzitunga Injili nzima sawa na matakwa yao walizieneza baina ya watu pasipo aibu, basi haikuwa vigumu kwao kubadili na kutoma yasiokuwemo katika kitabu chochote? Tena, ilipokubaliwa pia kwamba Injili hizi hazikuandikwa katika zama za Masihi, bali mkusanyiko wa Injili nne hizi ukatokea duniani miaka sitini au sabini baada ya kufa kwa Masihi, kwa mujibu wa hitilafu za masimulizi, hii pia inatia shaka zaidi kwenye ukweli wa Injili hizi. Kwani ni vigumu kuhakikisha kwamba wanafunzi walikuwa hai hadi muda huo, au nguvu zao zlibaki. Sasa, kwa kufupisha habari hizi zote, twawahakikishia wasomaji kwamba Wakristo hawajathibitisha barabara kwamba Injili kumi na mbili ni za bandia na zile nne wanazozieneza zimeepukana na uzushi na kutomwa maneno. Bali, wenyewe wanakiri kuhusu Injili hizi nne kwamba hizi nazo si maneno halisi ya Mungu. Na hata kama wasingekubali jambo hili, bado haikuwa shaka yoyote katika Injili hizi kughushiwa. Kwani ni jukumu lao kuthibitisha habari hii ambayo hawakuweza kuachiliwa kuwajibika mpaka leo kwamba kwa nini Injili zinginge ni za bandia lakini si hizi [nne].

watu wenye kutafakari huko Ulaya na Merikani. Na wao wanapendelea zaidi kubaki wakanamungu kuliko kumwamini mungu mwenye kasoro, mwenye kubadilika, na mwenye mwili, ambaye kwake Injili inaongoza. Basi, rafiki yangu mmoja Mwingereza msomi amenitaarifu kutoka Marekani kupitia barua mbalimbali kwamba hakuna mtu hata mmoja miongoni mwa wenye busara katika nchi hizo anayeamini kuwa dini ya Kikristo haina kasoro na dosari, na ambaye asiwe tayari kabisa kukubali Islam. Na ingawa Wakristo wameeneza tafsiri potofu za Kurani Tukufu kwa sura mbovu huko Ulaya na Marekani, lakini nuru iliyofichika ndani yao imeendelea kuiathiri mioyo iliyo safi. Ilmuradi, Marekani na Ulaya pana hali ya msisimko mkubwa siku hizi, na itikadi za Injili zilizo kinyume na uhakika zimewafadhaisha sana, hata kwamba wengine walidhihirisha rai hii kwamba hakuzaliwa kwa hakika mtu aliyeitwa jina Masihi au Isa, bali mradi wake ni jua, na wale wanafunzi kumi na wawili mradi wake ni buruji kumi na mbili [za falaki]. Tena, uhakika wa dini ya Kikristo unafichuka zaidi na jambo hili kwamba alama zile Hadhrat Masihi alizowawekea waaminio, miongoni mwao haipatikani hata moja katika watu hawa. Hadhrat Masihi alisema: Mkinifuata mtakuwa kivuli changu katika kila aina ya baraka na katika kukubalika, na ninyi mtapewa miujiza na ishara za kukubalika, na dalili ya

ukweli wa imani yenu itakuwa ni hii kwamba mtakuwa na uwezo wa kuonyesha ishara za aina aina, chochote mtakachotaka kitafanyika kwa ajili yenu, wala hakutakuwa na jambo lisilowezekana kwenu. Lakini, Wakristo hawana chochote mkononi mwao kutoka katika baraka hizi. Hawamjui yule Mwenyezi Mungu Anayesikia maombi ya waja wake mahususi, na Huwajibu ana kwa ana kwa upendo na rehema, na Huonyesha kwa ajili yao mambo mengi ya ajabu. Lakini Waislamu wa kweli walioshika mahali pa wanyofu wale na ni warithi wao waliopita kabla yao, wao wanamtambua Mungu Yule na wanashuhudia ishara za rehema Yake. Nao wanapambanuka dhidi ya wapinzani wao, mithili ya jua dhidi ya giza. Tumekwisha andika mara kwa mara kwamba dai hili lisifikiriwe kuwa pasipo dalili. Baina ya dini ya kweli na ya uwongo ipo tofauti moja mbinguni na moja ardhini. Tofauti ya kiardhi muradi wake ni ile tofauti inayofafanuliwa na akili ya mtu na dhamiri na kanuni asilia ya ulimwengu huu. Basi, dini ya Ukristo na Islam zikipimwa kwa kigezo hiki, inathibitika waziwazi kuwa Islam ni dini ya asili ambayo kanuni zake hazina kujisingizia wala kujikalifisha. Na amri zake siyo bidaa na za kubuniwa, na hakuna jambo linalokubalishwa kwa kulazimishwa. Na Alivyosema Mwenyezi Mungu Mwenyewe mara kwa mara, Kurani Tukufu inatukumbusha elimu zote za maumbile ya asili

na kweli zake, na hufichua siri zake za ndani, na haileti mambo mengine mapya yaliyo kinyume chake, bali kwa hakika hutufunulia maarifa yake ya undani. Lakini kinyume chake, mafundisho ya Wakristo, yanayonasibishwa kwa Injili, yanamtambulisha 'mungu' mpya na ambaye kwa kujiua kwake ndio unategemea ukombozi wa dunia kutoka katika dhambi na adhabu, na kwa kuteseka kwake ndiyo inategemewa raha ya mahuluku na kwa kubezwa na kudhalilika kwake ndio inafikiriwa heshima ya wanaadamu. Kisha imeelezwa kwamba yu 'mungu' wa ajabu kwamba sehemu moja ya umri wake imepita pasipokuwa na mwili na dosari za mwili, na sehemu ya pili ya umri wake (kwa sababu ya bahati mbaya isiyojulikana) yeye akafungwa ndani ya mwili kwa milele, na kiwiliwili, ngozi na mifupa na kadhalika vikawa vya lazima kwa ajili ya roho yake; na kwa sababu ya kuwa na mwili utakaodumu pamoja naye akalazimika kukabili taabu za anwai mbalimbali, hatimaye akafa kwa sababu ya kulemewa na mateso. Kisha akafufuka tena, na mwili ule ule tena ukamteka, nao utaendelea kumshika milele, na hataweza kuwa huru kamwe. Sasa angalieni je tabia njema inaweza kuikubali itikadi hii? Je dhamiri safi inaweza kutoa ushahidi wake? Je, hata sehemu tu moja ya kanuni ya asili inaweza kujuzu msiba na mateso hayo kwa Mungu Asiye na dosari na kasoro na Asiyebadilika kwamba kwa ajili ya kuumba kila

ulimwengu na kisha kuuokoa analazmika kufa mara moja, na Hawezi kudhihirisha sifa ya kutoa heri yoyote, wala Hawezi kuwafikishia raha yoyote viumbe Wake duniani au huko akhera bila kujiua. Ikiwa Mungu anahitaji kujiua ili kuwateremshia rehema viumbe Vyake, basi inamlazimu Yeye daima Akabiliane na msiba wa mauti, na Awe ameshaonja vifo tele hapo awali. Pia yamlazimu Awe amesitishiwa sifa Zake kama Parmeshar wa Mabaniani. Hebu fikirieni, je mtu mnyonge na dhaifu kiasi hicho anaweza kuwa Mungu, ambaye hawezi kuwapatia heri mahuluku wake wakati wowote na katika zama zozote bila kujiua kwanza? Je udhaifu na unyonge kama huo unamfaa Mungu, Mwenye nguvu zote? Kisha angalieni natija ya kifo cha mungu wa Wakristo, hakuna chochote. Maisha ya mungu wao yalipotea, lakini shetani hakuathirika vibaya wala kazi yake. Shetani huyo huyo na wafuasi wake wale wale waliokuwa hapo awali wapo sasa pia. Wizi, uporaji, uzinzi, mauaji, kuongopa, kunywa pombe[57], kucheza kamari, kupenda anasa za dunia, ukafiri, ushirikina,

[57] Kutokana na magazeti ya hivi karibuni, imebainika kwamba pauni 130,060,000 zinatumika katika Dola la Uingereza kwenye utengenezaji na unywaji wa mvinyo. (Mwandishi mmoja, M.A. aliandika): Matukio mamia ya kujiua yanatokea kwa sababu ya pombe mjini London. Na hasa mjini London pekee, miongoni mwa wakazi 3,000,000 pengine watu elfu kumi tu hawatakuwa

ukanaji Mungu, na dhambi nyingine nyingi zilizokuwepo kabla ya kusulubishwa kwa Masihi, hata sasa zipo kwa nguvu ile ile bali kwa kasi zaidi.

---

wanywaji pombe, waila wanaume kwa wanawake, wote, kwa furaha na uhuru hunywa pombe na hunywesha. Hakuna mkutano wa wakazi wa London, chama au mahafali ambapo isiandaliwe kwanza brandi, sheri na divai nyekundu. Mvinyo inachukuliwa kuwa sehemu ya lazima katika kila mkutano. Na ni la kushangaza kuwa makasisi na mapadre mashuhuri wa London, licha ya kujiita wenye dini, ndio wanywaji wa hali ya juu. Katika mikusanyiko yote kama hiyo ambako nimeshawhi kwenda kwa mwaliko wa Bw. Nichollette, humo baadhi ya mapadre vijana na wachungaji walionekana kabisa kushiriki. Mjini London kunywa pombe haichukuliwi kuwa ni jambo baya. Imeongezeka sana kunywa pombe hadharani, wakati nikizunguka London, niliona Waingereza wengi kwa macho yangu wakiyumbayumba wakiwa na chupa za mvinyo mikononi mwao. Kisia sawa na hii. Vilevile, wanawake walionekana wakitembea na chupa ya bia mjini London wakipepesuka. Niliona watu ma-ishrini wenye heshima zao wakiwa wameanguka kwenye mifereji ya maji machafu wakiwa wamelewa. Minajili ya unywaji wa pombe na 'baraka' zake matukio mengi ya kujiua hutokea mjini London kiasi kwamba kila mwaka janga lao kubwa la kuangamiza linachepuka. (Rahbare Hind, Lahore, 1 Februari, 1883)

Kadhalika bwana mmoja akitaja uzinzi wa mjini London uliozagaa na kuzaliwa kwa wanaharamu zaidi ya elfu sabini kwa kila mwaka ameandika mambo maovu ya watu hao ambayo kalamu haithubutu kuyaelezea. Baadhi yao wameandika na hili

Kwa mfano, angalieni mungu wa Wakristo bado alipokuwapo hai, Wakristo walikuwa katika hali nzuri. Lakini mara tu mungu huyo alipofikiwa na mauti

---

pia kwamba kama watu wastaraabu wa hali ya juu wa Ulaya wakigawiwa katika mafungu kumi, bila shaka mafungu tisa miongoni mwao watakuwa wakanamungu walioacha kufuata dini, kuamini uwepo wa Mungu Mwenye Enzi, na itikadi ya malipo ya wema na ubaya. Na siku hadi siku ugonjwa wa ukanaji Mungu unazidi kuenea katika Ulaya. Na inaonekana kuwa serikali ya Uingereza kwa sababu ya ukunjufu wa moyo, haikuchukizwa na kuendelea kuongezeka hili, hata kwamba baadhi ya wakanamungu kabisa wamepata viti bungeni, na haikujali hata kidogo. Kwa wanaume kuwabusu wasichana si tu imejuzu bali ni kitendo cha kusifiwa katika ustaarabu wa kisasa wa Ulaya. Hakuna awezaye kusema kwa yakini kwamba kuna mwanamke huko Uingereza ambaye hajawahi katika ujana wake kubusiwa na kijana mgeni. Uchu wa anasa za dunia umekithiri sana hivi kwamba Arope Alexander anaandika katika barua yake moja (aliyotuma kwangu) kwamba kwa maoni yake hakuna hata mmoja miongoni mwa wastaraabu na wasomi wa nchi hii anayeijali akhera, bali watu wote wamezama kabisa kabisa katika upendo wa anasa za dunia. Sasa ni wazi kutokana na kauli hizi zote kwamba athari zile za Masihi kutoa dhabihu, ambazo mapadre wanazihubiri wakija India, kwa watu wasiojua, ni uzushi mtupu wa hao mapadre. Na uhakika wenyewe ni huu kwamba kwa kukubali masiala ya kafara, tabia za Wakristo zimegeuka kwenye hii kwamba unywaji wa mvinyo umeenea sana, uzinzi na kutazama wanawake vimechukuliwa halali

yaitwayo kafara, tangu hapo shetani akawatawala watu hao kwa namna ya ajabu, na maelfu ya milango ya dhambi, uasi na kufuata matamanio ya nafsi ikafunguka. Na Wakristo wenyewe wanakiri ukweli huu, na Padre Pfander mtunzi wa kitabu cha *Mizan-ul-Hak* anasema kwamba kwa sababu ya kukithiri ndani ya Wakristo dhambi, na kuenea maovu ya ndani, na fuska baina ya Wakristo, Muhammad[saw] alitumwa kwa lengo la kuwaadhibu na kuwaonya Wakristo. Basi inadhihirika kutokana na maelezo haya kwamba tufani ya dhambi na uasi ilizuka katika Wakristo baada ya tu kusulubishwa kwa Masihi. Hii yathibitika kwamba kifo cha Masihi hakikuwa kwa shabaha hii kwamba mwendo kasi wa dhambi upungue. Mathalan, kama

---

kabisa, kucheza kamari imeongezeka kuvuka mipaka. Kumwabudu Mwenyezi Mungu kwa moyo wote na kuelekea Kwake, mambo haya yote yamekoma. Naam, ustaraabu kuhusu utawala bila shaka unapatikana hapo Ulaya. Yaani dhambi zilizo kinyume na maelewano ya wote, kama vile wizi, mauaji, ubakaji n.k., ambazo zimepigwa maarufuku na sheria za serikali ya kifalme kwa maslahi ya nchi, kweli zimezuiliwa. Lakini sababu ya dhambi kama hizo kuzuilika siyo kwamba kafara ya Masihi imeleta athari hii, bali hofu ya sheria na shinikizo la jamii limeathiri hivyo; kama visingekuwepo vizuizi hivyo mabawana Wakristo wangewahi kutenda hayo yote pasipo kujali. Tena, uhalifu huo wote unafanywa katika Ulaya kama unavyofanwya katika nchi nyinginezo, sio umefutuliwa kabisa. Mwandishi

watu walikuwa wamejikita katika unywaji wa pombe kwa wingi na uzinifu kabla ya kifo chake, au walikuwa wamependa sana anasa za dunia, basi siyo maana yake kuwa dhambi zote kama hizo zitatoweka baada ya kifo cha Masihi. Kwani, jambo hili halihitaji uthibitisho kwamba kiasi unywaji wa pombe, kufuata matamanio ya dunia na uzinzi ulivyoenea siku hizi, hasa katika nchi za Ulaya, kiasi kwamba hakuna mtu mwenye akili awezaye kufikiria kwamba kabla ya kifo cha Masihi tufani hii hii ya uwi na uovu iliendelea kwa kasi hiyo, bali haiwezi kuthibitishwa hata sehemu yake ya elfu. Na kwa kuzisoma Injili kwa makini yabainika kabisa kwamba Masihi kamwe hakutaka kukamatwa na Wayahudi na kupigwa na kutundikwa msalabani. Kwani, kama huu ulikuwa ni utashi wake basi kwa nini angeendelea kulia usiku kucha kwa kuepushwa balaa hiyo, na kwa nini angeomba akilia: "Aba, Baba, yote yawezekana kwako; Uniondolee kikombe hiki." Bali ukweli ni kwamba Masihi alikamatwa ghafla bila ya ridhaa yake, naye aliomba kwa kulia mpaka kufa kwake: Mungu wangu, Mungu wangu mbona umeniacha? [58] Hii yahakikisha kwamba Masihi alitaka kuishi na kukaa katika dunia hii kwa muda zaidi, kwa namna yoyote iwayo, na roho yake ikapapatika katika hali ya kufadhaika kwamba kwa

[58] Mathayo 27:46

vyovyote Maisha yake yasalimike. Lakini ikamfikia 'safari' hii kinyume na ridhaa yake. Ni la kutafakari pia kwamba Masihi amepata nini kwa kufa kwa njia hii kwa ajili ya kaumu yake ilivyopendekezwa na Wakristo, na kaumu yake imenufaikaje? Kama angeishi, angewaletea marekebisho makubwa watu wake, angewaondolea taksiri kubwa. Lakini kifo chake kilifaa nini isipokuwa kwamba mamia ya fitina zikazuka kwa kifo chake wakati pasipofaa, na ukatokea uharibifu uliofanya ulimwengu mmoja kuangamia. Ni kweli kwamba watu mashujaa hutoa maisha yao kwa watu wao, au wanayatia maisha hatarini kwa kuwaokoa watu wao, lakini si kwa njia hii ya kipuuzi na isiyofaa ambayo inaelezwa kuhusu Masihi. Bali anayetoa uhai wake kwa busara minajili ya kaumu, au kuutia hatarini, huchagua miongoni mwa njia zifaazo waziwazi njia iliyo bora na inayofaa dhahiri shahiri ya kujitoa maisha — njia ambayo kwa kuitumia ingawa yeye ateseke, au kugharimu maisha yake, lakini watu wake waokoke kikweli na baadhi ya balaa. Si kwamba ajiue kwa kujinyonga au kumeza sumu, au kujitupa ndani ya kisima, na kisha adhani kwamba kujiua kwake kutaileteа kaumu yake maendeleo. Kitendo kama hicho ni cha wapumbavu tu, si cha wenye akili na waaminio; bali kifo kama hicho hii ni haramu, na hakuna anayenuia kufanya hivyo isipokuwa jahili na mwendawazimu. Nasema kweli kwamba kufa kwa mtu mkamilifu shujaa — isipokuwa

katika ile hali maalum ambapo kulazmike kufa kwa njia ifaayo na maarufu kwa ajili ya kuwaokoa watu wengi — hakufai kamwe kwa watu wake, bali huwa ni msiba mkubwa na tukio la kuomboleza. Na mtu ambaye dhati yake inawanufaisha mahuluku wa Allah kwa anuwai mbalimbali, akiamua kujiua, atakuwa mwenye dhambi kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu, na dhambi yake itakuwa kubwa zaidi kuliko wakosefu wote wa namna hii. Hivyo basi, ni wajibu kwa kila mkamilifu, kujiombea kwa Mwenyezi Mungu maisha marefu, ili aweze kuyatimiza ipasavyo majukumu yake yote kwa ajili ya viumbe wa Mungu, ambayo kuyafanya ametiwa jazba moyoni mwake. Naam, kufa kwa mtu mshari ni afadhali kwake yeye mwenyewe na kwa viumbe wa Mwenyezi Mungu ili shari zisiendelee kuongezeka na viumbe wa Mungu wasije kuangamia kwa sababu ya shari yake ya kila siku. Na ikiulizwa kwamba kati ya Manabii wote, nabii yupi alijitia zaidi hatarini kwa kuwaokoa watu na kudhihirisha utukufu wa Mwenyezi Mungu kupitia njia ya busara na wakati ulipohitajika, na alitaka kutoa uhai wake kwa ajili ya kaumu — Masihi au Nabii mwingine au Seyidna na Maulana wetu Muhammad[saw] — basi jibu lake lilivyojaa kifuani mwangu kwa mshawasha wa hali ya juu sana na kwa hoja zing'aazo, aya zilizo bayana, na ushuhuda wa kihistoria, naliacha kuandika mahali hapa kwa msikitiko mkubwa, kwani li

refu mno, makala hii fupi haiwezi kubeba yale yote. Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu Akipenda na maisha yangu yakinijalia fursa, nitaandika kijitabu juu ya mada hii pekee. Lakini natoa habari njema hapa kwa ufupi kwamba yule mtu mkamilifu, mwenye kujitoa dhabihu nafsi yake kwa watu wake na kwa wanadamu wote ndiye Mtume wetu Mtukufu[saw], yaani سَيِّدُنَا وَ مَوْلَانَا وَ وَحِيْدُنَا وَ فَرِيْدُنَا أَحْمَدُ مُجْتَبَى مُحَمَّدٌ مُصْطَفَى الرَّسُوْلُ النَّبِيُّ الْأُمِّيُّ الْعَرَبِيُّ الْقُرَشِيُّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ[59]

Nimekwisha elezea kidogo ile tofauti iliyopo ardhini kwa kupambanua dini ya kweli na ya uongo, yaani mambo yanayoweza kuamuliwa kwa akili na dhamiri. Lakini ile tofauti inayopambanuka kwa mbingu nayo pia yalazimika kiasi kwamba bila hiyo haki na batili haviwezi kupambanuka. Nayo ni hii kwamba mfuasi wa dini ya kweli hupata uhusiano wa kipekee na Mwenyezi Mungu, na mfuasi mkamilifu huyo anakuwa dhihiriko la Nabii wake anayemfuata, na anakuwa mfano wa hali zake za kiroho na baraka za batini. Na kama vile mjukuu pia anaitwa mwana kwa sababu ya kiungo cha mwana, kadhalika mtu aliyelelewa chini ya ufuasi wa Nabii, naye hutendewa kwa hisani na baraka atendavyo Nabii

[59] Seyidna na maulana, wa pekee, asiye na kifani, Ahmad, Mteule, Muhammad Mchaguliwa, Mtume, Nabii Ummi Mwarabu Mkureishi, salamu na amani ziwe juu yake.

mwenyewe naye kama vile Nabii anaonyeshwa ishara, vivyo hivyo yeye pia hupewa ishara hasa kwa ajili ya kuongeza maarifa yake. Basi, watu kama hao wanakuwa ishara zilizo hai kwa ajili ya ukweli wa dini ambayo kwa kuisaidia wanadhihiri. Mwenyezi Mungu Huwasaidia kutoka mbinguni, na Hukubali maombi yao kwa wingi, na Huwajulisha kuhusu ukubalifu. Wanapata misiba pia siyo kuwaangamiza; bali, ili hatimaye ishara zionyeshwe kwa kuwasaidia hasa. Hao hupata heshima baada ya dhila, na huhuika baada ya kufa, ili kazi maalumu za Mungu zidhihirike ndani mwao.

Huku jambo hili linahitaji kuzingatiwa kwamba maombi yanakubaliwa kwa njia mbili: Kama *ibtilaa* [kwa kujaribu], na kama *istafaa* [kwa kuteuliwa]. Kama kujaribu baadhi ya wakati hata maombi ya watu wenye dhambi, waasi na pengine ya makafiri pia yanakubaliwa; lakini kukubaliwa hivi hakumaanishi ukubalifu halisi, bali kwa kutahini na kujaribu. Lakini dua inayokubaliwa kwa kuteuliwa inakuwa na sharti kwamba mwombaji lazima awe miongoni mwa wateule wa Mungu, na zidhihirike nuru na athari za ucha Mungu ndani mwake kutoka kila upande. Kwani, Mungu Mwenye enzi Hakubali kamwe maombi ya waasi kama ukubalifu hasa, bali Yeye Husikia maombi ya wale tu walio wanyofu machoni Pake na wanafuata amri Zake. Kwa hiyo, tofauti kati ya maombi kukubalika kwa kujaribu, na

kukubalika kwa maombi kwa kuteuliwa ni kwamba dua inayokubaliwa kama majaribio haina sharti la kuwa mcha Mungu na rafiki wa Mungu, wala haihitaji kwamba Mwenyezi Mungu kwa kukubali dua Ajulishe kuhusu kukubaliwa kwake kupitia maongezi yake matukufu, wala dua hizo hazina daraja ya juu kiasi kwamba kukubaliwa kwao kuweze kufikirika ya ajabu na isiyo ya kawaida. Lakini maombi yanayokubaliwa kwa sababu ya kuteuliwa yanakuwa na alama hizi dhahiri ndani yao:

(1) Kwanza, mwombaji huyo anakuwa mcha Mungu, mnyofu na mja mkamilifu.

(2) Ya pili, anafahamishwa kupokelewa kwa maombi yake kupitia maneno ya Mungu.

(3) Ya tatu, dua nyingi zinazokubaliwa huwa za daraja ya juu sana na zinahusiana na mambo magumu, ambazo kwa kupokelewa kwao inapambanuka kwamba hii sio kazi ya mtu wala mpango wake, bali ni mfano hasa wa kudura ya Mwenyezi Mungu unaowadhihirikia wateule wake mahususi.

(4) Ya nne, maombi ya majaribio hukubaliwa kwa nadra sana; lakini maombi ya uteuzi hukubaliwa kwa wingi sana. Wakati mwingine, mwombaji wa dua ya *kiistifaa* [uteuzi] hunasa katika matatizo makubwa ambayo angenasa humo mtu mwingine, asingepata njia ya

kujiokoa maisha yake isipokuwa kujiua. Na inatokea hivi pia kwamba watu waipendao sana dunia, walio mbali na Mwenyezi Mungu, wanapopatwa na huzuni na ghamu kubwa na maradhi na magonjwa na balia zisizotatulika, hatimaye kwa sababu ya udhaifu wa imani, kwa kukata tamaa na Mwenyezi Mungu, wanameza sumu au kuruka kisimani, au wanajiua kwa bunduki. Lakini, mwenye *istafaa* [uteuzi] katika nyakati ngumu kama hizo, kwa sababu ya nguvu ya imani na uhusiano wake mahususi husaidiwa na Mwenyezi Mungu kwa namna ya ajabu kabisa, na msaada wa Kiungu hushika mkono wake kwa njia ya ajabu hata kwamba mtu wa karibu yake hutamka kwa kushindwa kujizuia kwamba kweli mtu huyu anasaidiwa na Mwenyezi Mungu.

(5) Ya tano, mwombaji dua ya *kiistifaa* hushukiwa fadhili za Mungu, na Mwenyezi Mungu Huwa Msimamizi wake katika mambo yake yote. Na nuru ya upendo wa Mwenyezi Mungu, furaha ya utukufu wa kukubalika, na athari za kujaliwa ladha ya kiroho na neema hudhihirika usoni mwake, kama Asemavyo Mwenyezi Mungu:

تَعْرِفُ فِيْ وُجُوْهِهِمْ نَضْرَةَ النَّعِيْمِ [60] اَلَآ اِنَّ اَوْلِيَآءَ اللّٰهِ لَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَ لَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ۔ اَلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَ
كَانُوْا يَتَّقُوْنَ۔ لَهُمُ الْبُشْرٰى فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَ فِي الْاٰخِرَةِ ؕ لَا تَبْدِيْلَ لِكَلِمٰتِ اللّٰهِ ؕ ذٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ

[60] Utatambua marini ya neema katika nyuso zao. Al-Mutaffifiin 83:25

الْعَظِيْمُ [61] اِنَّ الَّذِيْنَ قَالُوْا رَبُّنَا اللّٰهُ ثُمَّ اسْتَقَامُوْا تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ الْمَلٰٓئِكَةُ اَلَّا تَخَافُوْا وَ لَا تَحْزَنُوْا وَ اَبْشِرُوْا
بِالْجَنَّةِ الَّتِيْ كُنْتُمْ تُوْعَدُوْنَ ۔ نَحْنُ اَوْلِيٰٓؤُكُمْ فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَ فِي الْاٰخِرَةِ ۚ وَ لَكُمْ فِيْهَا مَا تَشْتَهِيْٓ اَنْفُسُكُمْ
وَ لَكُمْ فِيْهَا مَا تَدَّعُوْنَ ۔ [62] وَ اِذَا سَاَلَكَ عِبَادِيْ عَنِّيْ فَاِنِّيْ قَرِيْبٌ ؕ اُجِيْبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ اِذَا دَعَانِ ۙ فَلْيَسْتَجِيْبُوْا
لِيْ وَ لْيُؤْمِنُوْا بِيْ لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُوْنَ ۔ [63]

---

[61] Sikilizeni hakika marafiki wa Allah hawana hofu wala hawahuzuniki, ambao waliamini na wakawa wacha Mungu. Wao wanazo habari njema katika maisha ya dunia na katika Akhera, hakuna mabadiliko katika maneno ya Allah; huo ndio ufaulu mkubwa. Yuunus 10:63-65

[62] Hakika wale wasemao, Mola wetu ni Allah, kisha wakaendelea kwa kudumu, huwateremkia malaika (wakiwaambia): Msiogope wala msihuzunike, na ifurahieni Pepo mliyokuwa mkiahidiwa. Sisi ni marafiki wenu katika maisha ya dunia na katika Akhera, na humo mtapata vitu zinavyovipenda nafsi zenu na humo mtapata mtakavyoviomba. Haa Miim 41:31-32

[63] Na waja wangu wakuulizapo juu Yangu, basi hakika Mimi nipo karibu. Nayaitikia maombi ya muombji anaponiomba, basi waniitikie na waniamini, ili wapate kuongoka. Al-Baqara 2:187

Habedari! Yaani ufahamu kwamba walio marafiki wa Mungu, yaani wanaompenda na kupendwa na Yeye, alama zao ni hizi: Hawana hofu ya kwamba watakula nini au watakunywa nini au watasalimika vipi na balaa fulani, kwani wao hupewa utulivu kutoka Kwake. Hawahuzuniki kwa yaliyopita, kwani wanajaaliwa subira. Alama ya pili ni kwamba wao wanayo imani, yaani huwa wakamilifu katika imani, na wanamcha Mungu, maana yake hujiweka mbali na mambo yaliyo kinyume na imani na utii. Alama yao ya tatu ni kwamba wanaendelea (kupokea habari

Sasa, yapasa kufahamu kuwa daraja ya kupendwa, kukubalika na Uwalii wa kweli, ambayo nimekwisha elezea alama zake kwa muhtasari, haiwezi kamwe

---

njema kupitia maongezi ya Mungu na kwa ruya njema) katika ulimwengu huu pia na ule mwingine vilevile. Hii ni ahadi ya Mwenyezi Mungu kuhusu wao, isiyoweza kuvunjika na hii hii ndyio daraja ipendwayo waliyojaaliwa. Yaani, waja mahususi wa Mungu, ambao ni marafiki zake, lazima wanapata sehemu katika mazungumzo na Mungu na ruya za kweli. Na alama kubwa ya Uwalii wao ni hii hii kwamba wawe wamejaliwa heshima ya mazungumzo na maongezi na Mwenyezi Mungu. (Hii ndiyo kanuni asilia ya Mwenyezi Mungu) kwamba wale ambao wakikataa miungu mingine, wamfahamu Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa ndiye Mola wao, na kusema Allah peke yake ndiye Mola wetu, (yaani, hatutarajii Mola mwingine yeyote), kisha wanakaa imara wakati wa majaribio (hata yatokee matetemeko makali namna gani, au zivume pepo kali, au litande giza zito, wasipate kuyumba, kubadilika, na kuhangaika, wakikaa imara kabisa) basi wanawateremkia Malaika (yaani wanapewa habari njema kwa njia ya ufunuo au ruya) kwamba, sisi tu marafiki zenu na walinzi na wasimamizi wenu katika dunia na Akhera, na mtapata kila mtakachotamani huko Akhera. Yaani, kama mkikabili shida kidogo katika dunia hii, msijali kwani huko Akhera huzuni zote zitakwisha na matamanio yote yatatimia. Mtu akisema, yawezekanaje mtu kupata huko Akhera chochote akipendacho, basi ninasema, hakuna budi kuwa hivyo, na hii hii ndiyo inaitwa wokovu. Waila mtu baada ya kupata wokovu akiendelea kutamani baadhi ya vitu na katika hamu yao akaendelea kusikitika na

kupatikana bila kumfuata Mtukufu Mtume[saw]. Na kama Mkristo au Mwaria au Myahudi akitaka kuonyesha athari na nuru za kukubaliwa kwa kushindana na mfuasi

---

kuhuzunika, lakini hakupata hivyo, basi ameokolewa katika nini, kwani bado anayo taabu ya aina fulani. Hivyo basi, ni lazima kwamba Janna, au Pepo, au ***Mukti Khana***, au ***Surg***, chochote paitwe mahali palipo nyumba ya ufanisi wa hali ya juu, panapaswa kuwa nyumba ambamo mwanadamu apate furaha safi kwa kila namna, na pasiwepo huzuni yoyote ya dhahiri au ya batini, na pasitawale uchungu wa ushinde wowote. Naam, ni kweli kwamba hakutakuwa na mambo ya kipuuzi na yasiofaa, bali hata utashi wa hayo hautazuka ndani ya mioyo mitakatifu, bali katika zile nyoyo takatifu zilizotakaswa na fikira za kishetani, matamanio yatazalika sawa na asili safi ya mwanadamu na ridhaa tukufu ya Mwumba, ili mwanadamu apate barabara ufanisi wake wa nje na ndani, wa kimwili na kiroho, na aitwe mwanadamu mkamilifu kwa dhihirisho kamili la vipawa vyake vyote. Kwani kuingiza Peponi sio kwa lengo la kufuta alama zote za kibinadamu, kama wanavyofikiria wapinzani wetu Wakristo na Waaria. Bali, shabaha yake ni kwamba alama zote za asili ya mwanadamu zing'ae kidhahiri na kibatini kwa namna ya ukamilifu, ili kwa kutoweka kabisa kwa kupita kiasi, yadhihirike vizuri yale mambo yaliyo ya lazima kwa upande wa maumbile ya kidhahiri na kibatini ya binadamu.

Na kisha Akasema: Waja wangu mahususi (walio wateule) watakapouliza juu Yangu na wakisema Yupo wapi, basi wajue kwamba Mimi Nipo karibu mno. Nasikiliza maombi ya waja wangu wenye ikhlasi. Mja wangu mwenye ikhlasi anaponiomba

mkweli wa Mtume[saw], haitawezekana kwake kamwe. Na njia ya wazi ya kutahini ni kwamba kama kumkabili Mwislamu mmoja mwema ambaye awe Mwisalmu mkweli na mfuasi kikweli wa Mtume Mtukufu[saw] akisimama mtu mwingine kama Mkristo n.k. kwa kushindana na akisema kwamba kadiri ishara yoyote ile itadhihiri kwako kutoka mbinguni, au kadiri siri za ghaibu zitafunuliwa kwako, au kadiri msaada utakaopewa kwa kukubaliwa maombi, au namna utakavyodhihirishwa mfano wa kudura kwa kudhihirisha heshima na utukufu wako, au kama utapewa ahadi ya neema maalumu kama utabiri, au kama utapewa habari za maonyo kuhusu mpinzani wako mtesaji, basi katika mambo haya yote, kitakachotokea kwa njia yako na utakachoonyesha,

---

(iwe kwa moyo au kwa ulimi), Nayasikiliza. (Hivyo ukaribu uko wazi), lakini yawapasa wajiweke katika ile hali ambayo kwayo Niwe Naipokea dua yao. Yaani, binadamu anakuwa kizuizi chake mwenyewe; anapojipeleka mbali kwa kuachana na hali ya utakaso, ndipo Mwenyezi Mungu Naye Hujiweka mbali naye. Na wanatakiwa kuwa na imani thabiti Kwangu (kwani maombi hupokelewa haraka sana kwa sababu ya nguvu ya imani). Kama wakifanya hivyo, watapata mwongozo, yaani Mungu Mwenye enzi Atakuwa pamoja nao daima, na fadhili na mwongozo wa Kiungu hautawaacha kamwe. Hivyo, kukubalika kwa maombi pia ni alama kubwa ya Mawalii wa Mungu. Basi, tafakari. Mwandishi

mimi nami pia nitakionyesha chote hicho, basi haiwezekani katu kwa mpinzani yeyote kuingia katika shindano kama hili, na hawatajitokeza kamwe, kwani mioyo yao inashuhudia kuwa wa kadhabu. Hawana uhusiano wowote na Yule Mungu wa kweli Aliye Msaidizi wa wacha Mungu na ni Rafiki wa wakweli, kama tulivyokwisha eleza kabla pia kwa kiasi fulani.

هٰذَا آخِرُ كَلَامِنَا وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ أَوَّلًا وَآخِرًا وَظَاهِرًا وَبَاطِنًا۔ هُوَ مَوْلَانَا نِعْمَ الْمَوْلَىٰ وَنِعْمَ الْوَكِيْلُ [64]

---

[64] Huu ndio mwisho wa kauli yetu. Na sifa zote njema ni za Allah, mwanzoni na mwishoni, kwa nje na ndani. Yeye ndiye Mola wetu, ni Mola Mwema Aliyoje, na Mlinzi Mwema Aliyoje.